

"JUMBE KATIKA LESO: MATUMIZI YA MBINU YA KUSUTA"

NA

AZIZA MKEAGAWA OMARA

**UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA**

YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI



A1500194A

University of Nairobi Library Thesis

2015

2015

UNGAMO


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kutosheleza mahitaji ya shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi..........Tarehe 25/11/2015.....
.....

AZIZA MKEAGAWA OMARA.


(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Isimu na Lugha.

Sahihi..........Tarehe 25/11/2015.....
.....

Dkt. Iribe Mwangi.

(Msimamizi)

Sahihi..........Tarehe 25/11/2015.....
.....

Dkt. Ayub Mukhwana.

(Msimamizi)

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu;

Bw. Omara A. Kalasinga

Na

Bi. Evelyn Manga Kalasinga

Walinfungulia mlango wa elimu na hawakuchoka kuniongoza na kunihimiza hadi kiwango hiki cha uzamili. Mungu awape maisha marefu.

Aila yangu;

Prof: Agnes W. Mwang'ombe

Kwa kunitia moyo na kunifahamisha umuhimu wa masomo. Asante kwa mchango wako, pengine ningekuwa nimebobeza na changamoto zilizonikabili.

Mwishowe kwa mwanangu mpendwa;

Leila Manga Adwar

Ulinipa kila sababu ya kuendelea na masomo yangu, na kunipa motisha wa kuikamilisha kazi hii. Asante kwa kunivumilia kwani nilikunyima muda wako mwingi ili kuweza kukamilisha kozi hii. Hata ingawa mchanga, naomba Mungu akupe uwezo wa kufuata nyanyo zangu katika masomo na hatimaye kutimiza ndoto yako.

SHUKRANI

Safari ya kuikamilisha tasnifu hii imekuwa yenye changamoto nyingi, lakini hatukufa moyo bali tulijikaza kisabuni kutokana na ushauri, mawazo na maelekezo ya watu kadhaa. Mchango mkubwa wa watu hawa ulipunguza uzito wa kazi hii.

Kwanza, natoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwezo katika kipindi hiki cha digrii hii ya uzamili na kuniwezesha kuikamilisha salama.

Shukrani nyingi ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Iribe na Dkt. Mukhwana. Asanteni kwa kujinyima muda wenu ili muweze kunihudumia kwa kunielekeza vilivyo. Nawashukuru kwa mawaidha, tahakiki na maelekezo ya kitaaluma ambayo yalinifaa sana katika kuikamilisha kazi hii. Mungu awaongeze hekima.

Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Isimu na Lugha kwa ushauri wao na maelekezo ya kiakademia katika kipindi cha usomi wangu katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Shukrani zangu ziwaendee Prof. Abdulaziz, Prof. Habwe, Prof. Kithaka wa Mberia, Dkt. Zaja, Dkt. Buregeya, Dkt. Kineene, Dkt. Mbatiah na Bw. Mungania.

Katika familia yangu, ningependa kuwashukuru wazazi wangu Bw na Bi Kalasinga, ndugu zangu Johari, Abae na Komora kwa kunishauri na kunihimiza kuendelea na masomo.

Namshukuru mpenzi wangu Don Adwar na mtoto wetu Leila Adwar kwa kunivumilia hadi nikahitimisha kozi hii.

Rafiki zangu haswa Donna Miyumo na wengine wote ambao siwezi kuwataja kwa majina nasema asanteni kwa mawaidha na kunihimiza kuendelea na masomo. Watu ambao ningependa kuwashukuru ni wengi lakini nasema asante kutoka moyoni mwangu.

IKISIRI

Katika utafiti huu tunalenga kuchanganua jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa tukiongozwa na nadharia ya Upole. Utafiti huu ulihusu jumbe za kusuta za lesu mjini Mombasa. Utafiti huu ulikuwa unachunguza haipotesia nne kwamba a) maudhui ya kusuta, umbeya na mapenzi yanatawala katika lesu mjini Mombasa, b) Lugha ya kitamathali hujitokeza katika mbinu ya kusuta katika kuwasilisha jumbe za lesu, c) Lugha sanifu ndiyo lugha inayopendelewa katika maandishi ya lesu mjini Mombasa na d) Kuna mitindo tofauti ya lugha inayotumika katika lesu mjini Mombasa. Data ilikusanywa kutoka maduka makuu ya lesu mjini Mombasa. Kutokana na data hii, sampuli ya jumbe 100 ilichaguliwa ili kuchanganuliwa. Data ilichanganuliwa kwa kutumia majedwali na vielelezo vya nambari na maelezo ya matokeo kujadiliwa. Utafiti huu umegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti na katika sura ya pili tumejadili kwa kina suala zima la lesu. Katika sura ya tatu tumeainisha maudhui na sura ya nne tukaainisha mitindo ya lugha iliyotumika katika jumbe za kusuta za lesu. Mwishowe tukatoa muhtasari, hitimisho, changamoto za utafiti, mapendekezo na matokeo ya utafiti katika sura ya tano.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	ii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI WA UTAFITI	1
1.0 UTANGULIZI	1
1.1 TATIZO LA UTAFITI.....	2
1.2 MALENGO YA UTAFITI.....	2
1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA	3
1.5 MSINGI WA NADHARIA	5
1.5.1 Dhana ya Upole	5
1.5.2 Nadharia ya umitindo ya Leech (1969)	6
1.6 NADHARIA TETE.....	7
1.7 MBINU ZA UTAFITI.....	7
1.7.1 SABABU ZA KUTEUA MADA	7
1.7.2 UKUSANYAJI DATA	8
1.7.3 MATOKEO	8
1.7.4 UCHANGANUZI WA DATA.....	9
1.8 UMUHIMU WA UTAFITI HUU.....	9
SURA YA PILI.....	10
FAFANUZI KUHUSIANA NA SUALA ZIMA LA LESO	10
2.0 UTANGULIZI	10
2.1 MAANA YA LESO	10
2.2 HISTORIA YA LESO	11
2.3 MAENDELEO YA LESO	12
2.4 JUMBE ZA LESO KATIKA MAWASILIANO.....	13

2.5 AINA ZA LESO	14
2.5.1 Kaniki.....	14
2.5.2 Merikani	14
2.5.3 Kisutu.....	14
2.5.4 Kisutu Cha Harusi	14
2.5.5 Kanga za Magharibi.....	15
2.6 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA LESO.....	15
2.6.1 Miundo ya Sentensi	16
2.6.2 Msamiati.....	17
2.6.3 Matumizi ya Takriri.....	19
2.6.4 Matumizi ya maswali ya balagha	19
2.7 Sababu za kushiriki katika uandishi wa jumbe za kusuta kupitia lesu.....	20
2.8 Hitimisho	21
SURA YA TATU	22
UAINISHAJI WA MAUDHUI YA JUMBE ZA KUSUTA KATIKA LESO	22
3.0 Utangulizi	22
3.1 Uainishaji wa jumbe kimaudhui katika jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa	22
3.2 Matokeo na Maelezo	29
3.3 Hitimisho	36
SURA YA NNE.....	37
UAINISHAJI WA MITINDO YA LUGHA ILIYOTUMIKA KATIKA JUMBE ZA KUSUTA ZA LESO.....	37
4.0 UTANGULIZI	37
4.1 Mitindo ya Lugha katika Jumbe za Kusuta za Lesu Mjini Mombasa.....	37
4.2 Lugha ya Kitamathali kama Mtindo katika Lesu zilizo na Jumbe za Kusuta ...	41
4.3 Ukiushi kama Mtindo.....	44
4.4 Hitimisho	46
SURA YA TANO.....	47

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	47
5.0 UTANGULIZI	47
5.1 Muhtasari	47
5.2 Hitimisho	47
5.3 Changamoto za utafiti	48
5.4 Mapendekezo	48
MAREJELEO	50
VIAMBATISHO.....	52
KIAMBATISHO A: DATA YA UCHANGANUZI	52
KIAMBATISHO B: BAADHI YA PICHA ZA KANGA	58

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA UTAFITI

1.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumeshughulikia utangulizi wa utafiti huu kwa jumla. Tumeangazia usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na vilevile nadharia tete. Tumeeleza pia umuhimu wa utafiti huu na kufafanua upeo na mipaka ya utafiti huu. Zaidi ya haya tumeangazia msingi wa nadharia na vipi utatumikizwa kwenye utafiti huu na kisha kubainisha yaliyoandikwa kuhusu mada tunayoitaftiti..Hatimaye tumeangazia mbinu za utafiti ambazo tutatumia katika utafiti huu.

Leso ni neno la Kiswahili lililotoholewa kutoka kwa neno la Kireno "*lecos*". Hanby na Bygott (1984) wanasema jina kanga lilitokana na watumwa wanawake walioshikwa katika pwani ya Afrika Mashariki ambao walitia nakshi vitambaa walivyofungwa navyo wakati wa kusafirishwa na hatimaye kuviita kanga kwa sababu ya kufananishwa na ndege anayeitwa kanga. Maneno haya mawili baadaye yalitumika kama visawe kumaanisha vazi lile lile moja.

Patel na wit (2011) wanaeleza lesu au kanga kama vazi la karne ya 19 lililovaliwa na wanawake kutoka pwani ya Afrika Mashariki na Zanziba. Wanawake hawa ndio walioendelea kubadili mapambo katika kanga na kulifanya kuwa vazi maarufu katika karne ya 20.

Baadaye maendeleo ya lesu yalifanyika kwa kuongezea jumbe na misemo katika mwaka wa 1910. Nyongeza hiyo ilifanywa na familia ya Kaderdina Hajee Essak waliotoka Zanziba na baadaye kukita kambi Mombasa. Lesu zake zilitambulika kwa alama ya *K.H.E- Mali ya Abdulla*. Kufikia sasa wanawake katika nchi nyingi hutumia lesu kama vazi.

East African Centre (2009) wanaeleza kuwa lesu huwa na semi, methali na hata vitendawili. Semi hizi huweza kueleweka katika muktadha wa kitamaduni na nyingi huelezea maisha ya wanawake wa Afrika Mashariki na mahusiano yao tata. Jumbe nyingi huwa fiche miongoni mwa wanawake kwa sababu ya mila na desturi zao.

Kwa muda wa miaka 140,kanga imekuwa mojawapo ya vazi maarufu katika pwani ya Afrika Mashariki (Hilger 1999). Kanga huuzwa kama vipande viwili vilivyofanana viitwavyo gora na kimsingi huwa vazi la mwanamke. Hilger anaendelea kusema kuwa

vazi hili limetumika kwa miaka mingi sasa kama njia ya kujieleza na hivyo basi kuwa njia ya kimsingi ya kupitisha jumbe miongoni mwa wanawake wa Afrika Mashariki. Kulingana na Parkin (2005) kanga ni vazi la kipekee na teule kwa jinsi lilivyo na misemo ya Kiswahili kama sifa yake ya kimsingi.

Kimsingi lesi ni kiwakilishi cha sauti za wanajamii. Wanajamii huandika maoni, mawazo au jumbe kuhusu maisha kupitia lesi. Hivyo basi kuziangalia jumbe katika lesi kutasaidia kuhamasisha jamii kuhusiana na masuala ibuka katika jamii.

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu unahusu uchunguzaji wa matumizi ya mbinu ya kusuta katika jumbe za lesi. Matumizi ya mbinu hii ya kusuta yanaonekana kujitokeza sana katika jumbe za lesi japo hakuna tafiti zilizofanywa kudhihirisha matumizi haya. Tafiti chache ambazo zimefanywa kuhusu lesi kama vile Patel na Wit (2011) chimbuko na historia ya lesi, Hanby na Bygott (1984) historia ya kanga ya pwani ya Afrika Mashariki, aina za lesi na hata jumbe zinginezo kama za dini, amani na hata siasa Atogo (2005). Hivyo basi kutokana na msaada wa tafiti hizo nilibaini kuwa baadhi ya wataalamu wamefanya tafiti chache kuhusiana na jumbe za lesi lakini hawajafanya utafiti kuhusu jumbe za kusuta katika lesi. Kutokana na kukosekana kwa tafiti kuhusu jumbe za kusuta, tafiti ameona kuwa hili ni tatizo na linahitaji ufumbuzi. Hivyo katika kutatua tatizo hili, utafiti utahusu uchambuzi wa data ya jumbe za kusuta kutoka maduka makuu ya lesi mjini Mombasa na kuchanganua data hiyo kwa kuangalia vipengele vya maudhui, lugha ya kitamathali na hata mitindo ya lugha iliyotumika katika kuziandika jumbe za kusuta za lesi.

Tafiti hii itaimarisha ufahamu wa mbinu ya kusuta katika jumbe za lesi na vilevile kwa kuiweka katika maandishi itakuwa ni hazina kubwa kwa kizazi kijacho na lugha ya Kiswahili kwa ujumla hivyo basi kufanikiwa kuziba pengo lililopo.

1.2 MALENGO YA UTAFITI

Utafiti huu unayo malengo yafuatayo:-

- i. Kuchunguza lugha inayopendelewa katika maandishi ya lesi mjini Mombasa.
- ii. Kutambulisha maudhui tawala katika jumbe za lesi mjini Mombasa.
- iii. Kuchanganua lugha ya kitamathali inayojitokeza katika mbinu ya kusuta.
- iv. Kuchanganua mitindo ya lugha inayotumika katika lesi mjini Mombasa.

1.3 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti wetu umejibana katika lesu mjini Mombasa japokuwa maeneo ya kufanya tafiti za lesu ni mengi mno. Mjini Mombasa kuna maduka makongwe ya kuuza lesu ikilinganishwa na maeneo mengine nchini Kenya. Katika uchunguzi huu tutajikita katika jumbe kwenye lesu zivaliwazo na wanawake na haswa lesu zenye jumbe za kusuta. Vile vile ni rahisi kunukuu jumbe za kusuta zilizoko kwenye lesu madukani ikilinganishwa na kuwapata wanawake wakiwa wamevalia lesu hizo. Pia tutahitaji data katika uasilia wake ili kupata maana iliyokusudiwa. Lesu tunazotarajia kutumia kama sampuli katika utafiti wetu ni zile za chapa ya *Mali ya Abdulla*, *Mali ya Francis* na *Mali ya Tanzania*.

Chapa hizi zimechaguliwa kwa sababu zinayo rekodi ya idadi kubwa ya ununuzi wa lesu ikilinganishwa na mali zingine. Hii ni kwasababu thamani ya lesu hizi imechukuliwa kuwa ya kiwango cha juu ikilinganishwa na thamani ya lesu zingine. Tumefanya uchaguzi huu tukichukulia kuwa mji wa Mombasa utakuwa kiwakilisho mwafaka cha miji mingine ya pwani ya Afrika Mashariki. Mji wa Mombasa una watu wenye mila na desturi ya uvaaji lesu hivyo idadi ya wanawake wenye kuvaa lesu ni kubwa ikilinganishwa na miji mingine.

Uchanganuzi wa lesu ni mpana, lesu huweza kuchanganuliwa kiantropolojia, kisaikolojia lakini utafiti wetu umejikita katika mwelekeo wa kiisimujamii.

Uchanganuzi wa mitindo ya lugha huwa mpana kwa hivyo katika utafiti wetu tumejikita katika matumizi ya tamathali na ukiushi wa kisarufi.

1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kazi zilizowahi kuandikwa kuhusu lesu si nyingi mno na tafiti chache pia zimefanywa hapa nchini Kenya. Hapa nchini Kenya yaliyoandikwa kuhusu lesu ni machache. Vilevile ni tafiti chache ambazo zimeandikwa kuhusu lesu nchini Kenya kwa lugha ya Kiswahili.

Mburu (2011) alitafiti kuhusu jumbe katika vibandiko vya matatu mjini Nyahururu. Mtafiti huyu alichunguza jumbe, mitindo ya lugha na kubainisha hadhira lengwa. Alitumia nadharia ya pragmatiki katika ujumla wake lakini utafiti wetu utatumia nadharia ya Upole na ile ya Umitindo. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani alichunguza jumbe katika matatu ilhali tunachunguza jumbe za kusuta kwenye lesu.

Hadhira lengwa ni tofauti katika tafiti hizi mbili na vilevile yeye alishughulikia mji mdogo wa Nyahururu nasi tutajikita katika mji wa Mombasa. Kazi ya Mburu itatufaa kwani itatupa mwanga katika uchanganuzi wa mitindo ya lugha.

Muthuri (2012) alitafiti kuhusu jumbe katika grafiti ya maktaba za Chuo Kikuu cha Nairobi. Alitumia nadharia ya utambulisho. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani alichunguza jumbe katika grafiti ya maktaba za Chuo kikuu cha Nairobi ilhali sisi tunachunguza jumbe za kusuta katika lesu na tunatumia nadharia ya Upole na ile ya Umitindo. Utafiti huu utatufaa kwani alitumia mbinu za kiisimu ambazo zitatusaidia katika uchanganuzi wa mitindo katika lesu.

Atogo (2011) alichunguza jumbe za amani katika lesu. Katika makala yake aliangazia masuala tofauti kama vile matumizi tofauti ya kanga. Atogo anaeleza jumbe kadhaa za amani katika lesu. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani aliangalia jumbe za amani nasi tutajikita katika jumbe za kusuta katika lesu. Mbali na hilo Atogo hakujikita katika nadharia yoyote ile maalum kinyume na utafiti wetu ambao unajikita katika nadharia ya Lakoff ya Upole na ile ya Leech ya Umitindo.

Yahya- Othman (1997) alitafiti kuhusu jumbe katika kanga na sauti ya wanawake katika jamii ya waswahili. Analiangazia suala la sauti ya mwanamke katika kazi yake na jinsi wanake katika jamii ya waswahili wanavyoithamini kanga kama njia ya mawasiliano. Amechunguza pia jinsi wanawake wa Zanzibari wanavyotumia jumbe katika kanga. Katika kazi yake Yahya anagusia historia ya kanga na jumbe za lesu katika mawasiliano kwa ujumla wake. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani sisi tumejikita katika jumbe za kusuta za lesu naye aliangalia jinsi sauti ya wanawake wa Kiswahili inavyojitokeza kupitia lesu.

Beck (2001) alitafiti kuhusu jukumu la kanga kama nyenzo ya mawasiliano. Katika utafiti wake aliangalia chimbuko la lesu na jinsi mawasiliano hukamilika kupitia lesu. Alitazama kwa kina maana fiche na wazi katika lesu na kueleza jinsi maana hizi ni kiungo muhimu katika jamii. Beck hakujikita katika nadharia yoyote ile bali sisi katika utafiti wetu tumejikita katika nadharia ya upole. Tumejikita katika jumbe za kusuta za lesu ilhali Beck alijikita katika jukumu la Kanga kama nyenzo ya mawasiliano.

1.5 MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Lakoff (1973) ya Upole. Hii ndio nadharia kuu lakini tutatumia pia nadharia ya Leech (1969) ya Umitindo. Nadharia ya Lakoff haitoi maelezo kuhusiana na dhana za mitindo. Nadharia ya Leech itatuwezesha kuchanganua mitindo ya matumizi ya lugha kama inavyojitokeza katika jumbe za kusuta za lesu tutakazoangalia.

1.5.1 Dhana ya Upole

Dhana ya upole ni pana mno kwa sababu inafumbata mambo mengi ndani yake. Watu wanapowasiliana hufanya hivyo kwa kuzingatia mila na desturi kuonyesha umahiri wao katika mawasiliano. Lakoff(1973) alitoa sheria mbili kuu katika udhibiti wa mawasiliano kipragmatiki:

1: Kuwa wazi.

2: kuwa mpole.

Kwa kawaida wasemaji hujaribu kuzitekeleza sheria zote mbili. Aidha kulingana na Lakoff sheria hizo mbili zikigongana basi upole hupaswa kujitokeza. Hii ni kwa sababu huwa muhimu katika mawasiliano ili kuzuia kukosana na wakati huo huo kupata uwazi katika mawasiliano.

Kanuni za kimsingi katika nadharia ya Lakoff ya upole ni:

- 1) Usilazimishe
- 2) Toa fursa ya kuchagua
- 3) Mfanye A ajihisi vizuri- fanya urafiki naye.

Kanuni hizi ni sahihi lakini zilizo tata kiutekelezi kwa sababu lugha hutoa njia fungamani au changamano za kujieleza. Kwa mfano kujieleza kwa njia zisizo za moja kwa moja kama vile “chakula ki tayari” hudhihirisha upole zaidi kuliko kujieleza kwa njia ya moja kwa moja kama vile “ungependa kula”. Sentensi ya kwanza inaonyesha upatanifu na kanuni ya 1, kwamba unazuia kuleta mwingiliano na mahitaji ya unayewasiliana naye hivyo basi kuweka mipaka ya mawasiliano. Katika utafiti wetu tutaangalia jinsi matumizi ya mbinu ya kusuta katika kuwasilisha jumbe kupitia lesu heweke mipaka ya mawasiliano.

Wazungumzaji wengi hujihusisha na kanuni ya 2 (toa fursa ya kuchagua) kwa kutumia njia banifu na ujielezaji wa kujikinga unaowaruhusu wasikilizaji kutunga na kuzuia mawazo yao. Kwa kutojieleza kinguvu, njia banifu na ujielezi wa kujikinga hukata makali ya makabiliano. Wazungumzaji huwapatia wasikilizaji fursa ya kuchagua kujibu aidha vizuri au vibaya. Tunaazimia katika utafiti wetu kuchanganua jinsi matumizi ya mbinu ya kusuta hutumia njia banifu na ujielezi wa kujikinga katika kufumba maana zikusudiwazo kuwasilishwa.

Kanuni ya 3 (mfanye A ajihisi vizuri-fanya urafiki naye) hutumika sana katika maana za kitamaduni. Hujumlisha kanuni zote za Lakoff, yaani wanaowasiliana hugawa tabia na itikadi sawa katika mawasiliano kwa madhumuni ya kutathmini mawasiliano kulingana na kinachosemwa.

Tumedhamiria kubainisha upolekwa kuchunguza jinsi matumizi ya mbinu ya kusuta katika kuwasilisha jumbe kupitia lesi hufumba maana. Vile vile tumegundua kwamba nadharia ya upole ya Lakoff haitoi maelezo kuhusiana na dhana za mitindo na kwa sababu hiyo tutatumia nadharia ya umitindo ya Leech(1969) ambaponadharia ya umitindo itatuwezesha kuchanganua mitindo ya matumizi ya lugha kama inavyojitokeza katika jumbe za lesi tutakazoangalia. Kwa msingi huu tunaona kuwa nadharia hizi mbili kwa ushirikiano zitatuchanganulia data yetu kuhusiana na jumbe za kusuta katika lesi.

1.5.2 Nadharia ya umitindo ya Leech (1969)

Leech anatazama matumizi ya lugha kimitindo katika viwango vitatu vikuu:

- a) Kiwango cha utendaji
- b) Kiwango cha umbo
- c) Kiwango cha semantiki.

Kiwango cha utendaji kinahusu namna lugha inavyotamkwa na kuandikwa. Mjuzi wa lugha lazima awe na ujuzi wa kutamka na kuiandika lugha hiyo. Kwa ajili ya kazi yetu, tuangalia jinsi jumbe katika lesi zilivyoandikwa.

Kiwango cha umbo kinahusu msamiati uliotumika kujenga sentensi kwa kugemea mambo ya sarufi na leksia. Mtu anastahili kujua msamiati wa lugha na sheria ambazo zinaongoza mpangilio wa msamiati huo katika sentensi. Katika sehemu ya leksia

tunachunguza matumizi ya msamiati. Tutachunguza namna waandishi wa jumbe za lesi wameteua maneno yao katika maandishi. Watunzi huwa huru katika uteuzi wao na wanaweza kutumia maneno ya kilahaja, ya kale, ya kigeni, kuhamisha ndimi na pia kutumia sajili mbalimbali.

Katika kiwango cha semantiki tunaangalia jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Tunachunguza namna tamathali za lugha zinavyoathiri maana katika matini. Katika utafiti wetu tutabainisha mbinu mbalimbali za kitamathali zitakazojitokeza katika jumbe za lesi tutakazoangazia. Hii ni kwa sababu tamathali za usemi humwezesha mtunzi kusema mambo mengi kwa njia fupi yenye mvuto na mnato.

1.6 NADHARIA TETE

- i. Maudhui ya kusuta, umbeya na mapenzi yanatawala katika lesi mjini Mombasa.
- ii. Lugha ya kitamathali hujitokeza katika mbinu ya kusuta katika kuwasilisha jumbe katika lesi.
- iii. Lugha sanifu ndiyo lugha inayopendelewa katika maandishi ya lesi mjini Mombasa.
- iv. Kuna mitindo tofauti ya lugha inayotumika katika lesi mjini Mombasa.

1.7 MBINU ZA UTAFITI

Katika sehemu hii tunaangalia njia za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data hiyo ikifuatwa na ufafanuzi wa uchanganuzi huo. Njia ya kimsingi ni utafiti nyanjani.

1.7.1 SABABU ZA KUTEUA MADA

Tafiti kuhusu lesi ni chache ikilinganishwa na tafiti zingine zinazohusu aina zingine za mavazi. Ni sababu hii iliyonipa msukumo wa kutaka kufahamu kuhusiana na jumbe zilizopo katika lesi.

Msukumo mwingine ulionipelekea katika kutaka kutafiti mada hii ni kuwa sharti kulikuwa na masuala yaliyosababisha wanawake kutaka kuvalia lesi zenye jumbe za kusuta na ningependa kujua kwa nini.

Tulichagua mada hii kwa sababu matokeo yake yatachangia pakubwa katika lugha ya kiswahili kwani ni tafiti chache ambazo zimefanywa kwa lugha ya kiswahili.

1.7.2 UKUSANYAJI DATA

Tunaazimia kukusanya data kutoka duka kuu la lesi lililoko barabara ya lesi mjini Mombasa. Lesi tutakazotumia kama sampuli ni zile za Mali ya Abdulla, Mali ya Francis na Mali ya Tanzania. Tutakusanya data kwa kuangalia lesi 200 katika mali hizi tatu. Tutaangalia maandishi na tujanakili kwenye kitabu ili kufanya uchanganuzi. Ukusanyaji data unatarajiwa kufanyika kwa kipindi cha miezi miwili.

Njia nyingine ya ukusanyaji data ni upigaji picha. Tutapiga picha za lesi zenye jumbe za kusuta ili kuonyesha ithibati ya usahihi wa data ambayo tutakusanya. Data tutakayokusanya kutoka lesi ni data inayohusiana na jumbe zinazoonyesha matumizi ya mbinu ya kusuta.

Kudurusu vitabu maktabani na kutafiti katika mtandao kumetufaidi kwani kumetuwezesha kupata yaliyoandikwa kuhusu mada hii pamoja na msingi wa nadharia ya utafiti huu.

Zaidi ya haya tutafanya mahojiano ya moja kwa moja na watunzi wa jumbe hizi. Watunzi wa jumbe hizi huwa katika makundi kadhaa. Kuna wenye maduka. Hawa huwa wamiliki wa chapa haswa na utawapata pale madukani wakati wowote. Kundi lingine ni wale wanaokuja tu kuleta jumbe ili kupata malipo. Mahojiano na watunzi wa jumbe kuhusu misamiati fiche yatatusaidia kupata maana za baadhi ya misamiati na istilahi ambazo hatutakuwa tunafahamiana nazo. Matokeo ya mahojiano haya yataandikwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya uchanganuzi.

1.7.3 MATOKEO

Jumbe 200 zitakusanywa kutoka duka kuu la lesi mjini Mombasa na kuainishwa kama ifuatavyo:

- a) Jumbe 100 za Mali ya Abdulla
- b) Jumbe 50 za Mali ya Francis
- c) Jumbe 50 za Mali ya Tanzania.

Data tutakayokusanya ni nyingi kwa hivyo tutajikita katika sampuli ya data kutoka kwenye lesi mia moja. Lesi hizo ni kama ifuatavyo:

- a) Lesi 50 za Mali ya Abdulla

- b) Leso 25 za Mali ya Francis
- c) Leso 25 za Mali ya Tanzania

Sampuli za data zinatafautiana ambapo data kutoka mali ya Abdulla itakuwa nyingi ikilinganishwa na mali zingine tuliyoteua kwa sababu Mali ya Abdulla ndio iliyo na idadi kubwa ya wanunuzi wa lesu na tena ndio mali kongwe kwa mali zingine.

1.7.4 UCHANGANUZI WA DATA

Data tutakayokusanya tutaichanganuakwa kutumia nadharia ya Lakoff ya upole kama nadharia kuu ikisaidiana nay a umitindo ya Leech. Tutachukua hatua kuziainisha jumbe katika maudhui mbalimbali, pia tutachunguza lugha inayopendelewa katika uandishi wa jumbe za lesu. Mwishowe tutachanganua mitindo ya lugha inayojitokeza katika lesu kama vile tamathali za lugha na ukiushi. Tutafanya uchanganuzi huu kwa kutumia majedwali,vielelezo vya nambari na kisha kutoa maelezo mwafaka.

1.8 UMUHIMU WA UTAFITI HUU

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa kama kirejelewa kwa watafiti wa baadaye.

Utafiti huu utachangia usomi wa Kiswahili kwani ni tafiti chache zilizofanywa kuhusu jumbe za lesu kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya tafiti zilizofanywa za lesu ni kuhusu chimbuko na historia ya lesu,(Patel na Wit 2011),Hanby na Bygott (1984),historia ya kanga ya pwani ya Afrika Mashariki na aina na jumbe za dini,amani na siasa,Atogo (2005). Katika kutafiti jumbe za kusuta za lesu na kuhifadhi katika maandiko kutachangia usomi wa Kiswahili na jamii na utamaduni kwa ujumla. Matokeo yake yataleta ufahamu zaidi wa jumbe za kusuta za lesu na umuhimu wake katika jamii ya Kiswahili.

Utafiti huu utachangia pakubwa katika kuhamasisha jamii kuwa makini katika jumbe za lesu kwani huwa na jumbe nzito kuhusu maisha. Kuhifadhi matokeo kuhusu jumbe za kusuta za lesu kutasaidia katika kuhamasisha jamii katika kutilia maanani jumbe za lesu ikichukuliwa kuwa wengi wanaovalia vazi hili mara nyingi hawatilii maanani jumbe bali vazi lenyewe.

Matokeo ya uchanganuzi wa mitindo ya lugha yatasaidia katika usomi wa mitindo Kiisimu.

SURA YA PILI

FAFANUZI KUHUSIANA NA SUALA ZIMA LA LESO

2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tumeliangazia suala zima la lesu. Kwanza, tumeeleza maana ya lesu kutokana na maoni ya wataalamu mbalimbali. Pili tukaeleza historia ya lesu na pia kufafanua maendeleo ya lesu tangu enzi za kale. Vilevile tumejadili aina tofauti za lesu na hatimaye kuonyesha matumizi ya lugha katika lesu.

2.1 MAANA YA LESO

Lesu ni neno la Kiswahili ambalo limetoholewa kutokana na neno la Kireno “lecos”, pia huitwa kanga.

Hamid (2009)-Anaeleza kanga kama kipande cha nguo kilicho na ujumbe mzito unaovutia jinsia ya kike. Anaongeza kuwa kitamaduni rangi katika kanga huwa na maana maalum kwa mfano wanawake huvalia kanga za rangi nyekundu na nyeusi wakati wa hedhi. Hii ilikuwa ishara ya tahadhari kwa mwanaume wasiweze kuwaomba bidhaa.

African Liz (2009)- wanaieleza kanga kama kipande cha nguo ya kitamaduni kutoka Afrika Mashariki kilicho na upana unaoitwa pindo ,sehemu ya kati inayoitwa mji na ujumbe vyote vimeshonwa pamoja kwa nakshi nzito na rangi za kupendeza. Hii ni kumaanisha kuwa kanga au lesu hugawika sehemu na huwa na jumbe mbalimbali na kunakishiwa kwa rangi nzuri nzuri.

Hanby na Bygott (1984)-Wanaeleza kanga kama kipande cha nguo kilichotengenezwa na nyuzi kutokana na pamba kilicho na pindo na chenye nakshi nzito na rangi za kupendeza. Hawa vile vile wanakubaliana na African Liz (2009) katika maelezo yao ya lesu.

Hassan na Kassim (2004)- kanga imetokana na kitenzi cha zamani cha Kibantu ku-kanga kilicho na maana ya kujitanda au kufunga. Ni kitambara cha kupendeza kilichofanana na kitenge kinachovaliwa na wanawake na mara nyingine wanaume wa Afrika Mashariki. Kutokana na maelezo haya kanga si mali au vazi la wanawake pekee bali hata wanaume. Yamkinika waandishi hawa wanakichukulia kikoi kama aina ya kanga.

Mtandao wa East African Centre (2009) unaeleza lesu kama kipande cha nguo kilicho na pindo na nakshi nzito na rangi za kupendeza na chenye ujumbe chini yake. Urefu wake huwa kama mikono miwili iliyonyoroshwa na upana wake huweza kufinika shingo hadi magoti ama kiuno hadi viganja vya miguu. Maelezo haya yanasisitiza yaliyosemwa hapo juu kuhusu lesu kwa kuongezea dhana ya urefu na upana wake na pale ambapo maandiko yafaa kuwa, chini na wala sio juu.

Juki (2009)- Kitambaa kilicho kuja na chimbuko la biashara ya utumwa katika pwani ya Afrika Mashariki lakini maendeleo yake yameifanya kuwa vazi maarufu Afrika kwa ujumla. Juki hapa anadokezea historia ya vazi hili la kanga.

Linnebuhr (1994) – Lesu ni Kitambaa cha nguo kinachotumika kama nguo ya wanawake kote Afrika mashariki. Kitambaa hicho huwa na urefu wa sentimita 110 na upana wa 150. Hutambulishwa kwa pindo, mji na ujumbe chini yake. Chimbuko lake ni miaka ya 1880 Zanzibari.

Kulingana na maelezo tofauti ya kanga au lesu tunaweza kusema kuwa kanga ni aina ya vazi la wanawake lililo na nakshi na rangi za kupendeza, na hugawika katika sehemu tatu, ile ya upana inayoitwa pindo, ya kati ijulikanayo kama mji na shemu ya chini iliyobeba ujumbe.

2.2 HISTORIA YA LESO

Lesu au kanga ina historia ndefu kwani kuna mitazamo tofauti inayohusiana na chimbuko la vazi hili. Vilevile tamaduni ambazo zinahusishwa na lesu zimekuwepo kwa miaka mingi na bado zinaendelea kupata umaarufu.

Kanga imeelezwa kama vazi maridadi lililotengenezwa na kipande cha nguo kilicho katika gora na chenye ujumbe fulani (Patel na Wit 2011). Patel na Wit wanaeleza kuwa chimbuko la kanga lilitokana na biashara ya utumwa katika karne ya 19. Watumwa wanawake walioshikwa katika eneo la Afrika Mashariki walifungwa na kanga kabla ya kusafirishwa hadi nchi za kiislamu zilizoko Mashariki ya Kati. Waandishi hawa wasema awali kitambaa hicho kilikuwa cha rangi nyeupe lakini baadaye wanawake wakaanza kutia nakshi kwa vitambaa hivyo kwa kuongeza rangi zengine kwa kutumia mimea na mizizi.

Katika biashara hiyo ya watumwa wafanyibiashara kutoka Gujerati (India) walianza kusambaza vitambaa vyeusi vilivyojulikana kama “kaniki” vilivyovaliwa na

watumwa na wanawake wa hadhi ya chini. Wanawake wa hadhi ya juu kwa upande mwingine walipendezwa na vitambaa vilivyojulikana kama Merikani. Mapambo zaidi yaliongezwa katika miaka ya baadaye na vazi hili likaweza kupata jina *kanga* kutokana na kufananishwa na ndege anayejulikana kwa jina hilo. Kama lilivyo vazi hili, ndege ajulikanaye kama kanga ana rangi za kupendeza macho.

Hanby na Bygott (1984) wanaeleza chimbuko la kanga kama pwani ya Afrika Mashariki katika karne ya 19. Wanaeleza kuwa wanawake kutoka Zanziba walinunua vitambaa vilivyoitwa "*kerchiefs*" na kuvishona pamoja kutengeneza kitambaa kilichoitwa lesu. Vitambaa hivyo vililetwa na wanabiashara Wareno. Mkabala huu unaochukuliwa na Hanby na Bygott unakinzana na mawazo ya Patel na Wit.

Charles (1873) katika kitabu chake "*Life, wanderings and labours in Eastearn Africa*" anaeleza kuwa wanawake wa Mombasa walianza mtindo mpya wa kushona mitandio pamoja kutengeneza walichokiita lesu.

Troagher (1875) mwanahabari kutoka Australia anaunga mkono mawazo ya Charles kuwa madai ya kanga kutoka Zanzibari si kweli. Kwa maoni yake Zanzibari ilikuwa tu ni mahali ambapo wafanyibiashara wahindi walitengeneza na kuuza vitambaa vyao.

Kulingana na maelezo ya wataalamu tofauti kuhusiana na historia ya kanga tunaona kuwa vazi hili lilitokana na biashara ya utumwa katika karne ya 19. Japo wataalamu wengine wanatafautiana kuhusu chimbuko la vazi hili ni kweli kuwa kanga imebadilika kiwakati na kupata umaarufu Afrika Mashariki na kote ulimwenguni.

2.3 MAENDELEO YA LESO

Maendeleo ya lesu yalianza kufanywa na wanawake kutoka pwani ya Afrika Mashariki na Zanzibari kwa kubadili mapambo katika kanga na kulifanya kuwa vazi maarufu katika karne ya 20. (Patel na Wit 2011). Wareno walivutiwa na kazi hii na kuanza kutengeneza aina tofauti za kanga walizoita "*lecos*". Baadaye kanga na lesu zikaungana pamoja na maneno haya mawili kutumika kama visawe.

Maendeleo ya aina nyingine yalitokana na utengenezaji wa lesu kwa mashine. Lesu zilizotengenezwa kwa mashine zilitoka Marekani, Japani na Uchina. Hii ni kwa sababu mapinduzi ya viwandani yalianzia nchi za kimagharibi kabla ya kufika huku Afrika Mashariki.

Kulingana na Bygott na Hanby (1984) maendeleo ya lesu yaliongezeka kwa kiasi kikubwa katika karne ya 19. Maendeleo yalikuwa kuongezea jumbe na misemo katika lesu mwaka wa 1910. Jambo lililofanywana aila ya Kaderdina Hajee Essak waliotoka Zanzibari lakini baadaye kukita kambi Mombasa. Kanga zake zilitambulika kwa alama ya K.H.E-Mali ya Abdulla. Lugha iliyotumika ilikuwa ni ile ya Kiswahili lakini maandishi ya kiasilia yalikuwa ya Kiarabu. Misemo na jumbe hizo zilikuwa na maana kwa aliye vaa na msomaji. Jumbe hizo ziliaminiwa kutatua tatizo la mawasiliano katika tamaduni pale ambapo sauti za wanawake hazikusikika yaani ilikuwa ni jumbe kwa waliokandamizwa katika jamii.

Hassan na Kassim (2004) wanaeleza kuwa mapambo katika kanga yameendelea kubadilika kadri miaka inavyosonga kutoka nakshi kidogo hadi nakshi nzito za aina na rangi mbalimbali. Kanga inazidi kubadilika jinsi mavazi mengine kama mashati yanavyobadilika na kwa hivyo mabadiliko katika lesu yanazidi kupata umaarufu na matumizi yake kuongezeka kisiasa, kidini na hata kwa shughuli za kila siku. Katika sanaa vilevile kanga imekuwa kiungo muhimu kwa utamaduni wa Afrika Mashariki. Hii ni kwa ajili ya jinsi vazi hili litumiwavyo katika kazi za kisanaa kama uigizaji, katika nyimbo za kitamaduni miongoni mwa wanajamii wa pwani ya Afrika Mashariki na hata kama mapambo nyumbani.

Baadaye, mitazamo kuhusu lesu ilianza kubadilika. Wengine wakaanza kuiona lesu kama vazi la kupendeza, wengine wakaiona kama kiungo cha kubeba historia ya jamii, wengine kama utamaduni na wengine kama chombo cha kuelimisha jamii. Ni kwa misingi hii ambapo hapa chini tunatazama aina mbalimbali za lesu.

2.4 JUMBE ZA LESO KATIKA MAWASILIANO

Kazi ya lesu kama njia ya mawasiliano imejadiliwa na wataalamu tofauti wakiwemo (Beck 1995, Hamid 1995, Hillal 1989, Riyami 1989). Kwa ufupi jumbe za lesu zinajulikana kumiliki usemi. Sifa mojawapo ya usemi ni kuwa huwa na wanaosema na wanaosemewa. Jumbe za lesu ni semi za kijumla na pia semi maalum. Semi za kijumla huwa na hadhira pana yaani mtu yeyote atakayekutana na jumbe ya lesu huisoma na kuweza kuichanganua jumbe hiyo kwa namna anavyoielewa. Kwa mfano jumbe za lesu huweza kusomwa na mpita njia.

Kwa upande mwingine semi maalum hudhamiriwa kwa mtu binafsi na ujumbe huwa umeelekezwa kwa mtu binafsi kwa njia mbili ; kwanza lesu yenye ujumbe

mwafaka huweza kutumwa kama zawadi kwa mtu binafsi na aghalabu hakuna tashwishi kuhusiana na aliyeituma lesu yenyewe. Anayeipokea lesu huipokea lesu pamoja na ujumbe wake. Ujumbe wa lesu hapa mara nyingi huwa wa kumtakia mema mfano, “bora kupata kuliko kukosa au “subira ufunguo wa peponi” pili, lesu huweza kuvaliwa na fikra za mtu fulani akilini. Anaye valia lesu huvaa aidha akijuwa kuwa atakutana na anayemkusudia ujumbe huo mahali au marafiki zake.

2.5 AINA ZA LESO

Maendeleo ya lesu katika viwango mbalimbali yaliibua aina tofauti za lesu na kwa sasa aina hizi huvaliwa na makundi tofauti katika jamii jinsi zilivyovaliwa miaka ya nyuma.

2.5.1 Kaniki

Hii ni aina ya lesu za kwanza kutokea. Kaniki ni nyeusi na ilivaliwa na watumwa na wanawake wa hadhi ya chini. Kaniki iliingizwa Afrika Mashariki na wafanyikazi kutoka Gujerati India. (Patel na Wit 2011).

2.5.2 Merikani

Aina ya lesu nyeupe iliyovaliwa na wanawake wa hadhi ya juu wa Afrika Mashariki. Miaka ya baadaye Merikani iliongezwa nakshi kwa rangi nyekundu juu ya ile nyeupe na kuifanya kuwa vazi maridadi lililopata umaarufu miongoni mwa wanawake wa Afrika Mashariki na ulimwengu kwa ujumla.. (Patel na Wit 2011)

2.5.3 Kisutu

Aina ya lesu ambazo huwa na rangi nyekundu na nyeusi ama rangi nyeusi na samawati. Aina hii ni baadhi ya lesu zilizopata umaarufu Afrika Mashariki haswa Zanzibar.(Hanby na Bygott 1984)

2.5.4 Kisutu Cha Harusi

Aina hii hufanana na Kisutu na rangi zake huwa kama zile za Kisutu yaani nyekundu na nyeusi lakini huwa zimeongezwa nakshi kwa kiasi fulani. Kisutu cha harusi hutumika sana Zanzibar kuwatanda bibi harusi wakati wa harusi.

2.5.5 Kanga za Magharibi

Aina hii ya kanga huja kwa rangi ya samawati na nyeusi nzito na mchanganyiko wa rangi zingine. Aina hii ilipata jina hili kwani nakshi na rangi zake zilitokana na wanawake walioishi upande wa magharibi ya Zanzibar.

(Patel na Wit 2011) wanadai kuwa aina hizi mbalimbali za lesu zinazidi kupata umaarufu katika pwani ya Afrika Mashariki na kwingineko na kuendelea kulifanya vazi hili kuwa vazi teule miongoni mwa wanawake wa pwani ya Afrika Mashariki.

Aina hizi mbalimbali za lesu zinaashiria jinsi maendeleo ya lesu yalivyofanyika kutokea kitambaa cheupe,cheusi hadi kilivyopata naksi nzito nzito na rangi tofauti.

2.6 MATUMIZI YA LUGHA KATIKA LESO

Maandishi katika lesu hujitosheleza kufanikisha mawasiliano ambapo msomaji huweza kupata ujumbe bila kuhitaji ufafanuzi. Kila ujumbe katika lesu huwa umetengewa hadhira fulani na hueleweka miongoni mwa jamii fulani. Lesu huwa ni mfumo wa ishara ambao una mpangilio maalum. Ishara hii ya lesu huwa na vipashio kama mofu,maneno,virai,vishazi na hata sentensi. Vipashio hivi hupangwa ili kuleta maana katika mawasiliano.

Waandishi wa lesu mara nyingi hawajulikani. Mwenye duka katika duka la lesu la Mali ya Abdulla, Muneeb ambaye pia ni kitukuu cha Kardedina mwazilishi wa jumbe katika lesu anatumia kuwa waandishi wa lesu huwa wa aina tofauti,kuna wale wanaoleta jumbe dukani kutoka nje na jumbe zinapokubaliwa,hulipwa kiwango fulani cha pesa. Asilimia kubwa ya jumbe huwa wametunga wenyewe.

Felix Mwaro kutoka duka la mali ya Francis anaeleza kuwa asilimia 80% ya jumbe zao hutunga wenyewe wakishirikiana na wafanyikazi dukani na asilimia 20% hutoka kwa wanunuzi. Jambo hili huwapa waandishi uhuru wa kuandika jumbe bila viziuzi vyovyote na hali hii huibua lesu zenye jumbe nzito na ubunifu mwingi.

Waandishi wa lesu pia aghalabu huwa hawafungwi katika sheria za kiisimu jambo ambalo huwapa uhuru na nafasi ya kuonyesha ubunifu wao. Hapa tumeangazia jinsi waandishi katika lesu hutumia lugha katika uandishi wao.

2.6.1 Miundo ya Sentensi

Massamba (2009) anaeleza sentensi kama kipashio cha tungo kikubwa kabisa cha kimiundo chenye maana kamili. Katika kazi hii tumeshughulikia miundo ya sentensi kama vile, sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano.

- **sentensi sahili/ Vishazi**

Sentensi sahili huwa na muundo wa kiima kimoja na kiarifu kimoja, Kamusi sanifu ya Isimu na Lugha (1990). Kwa mfano;

Mf. 1

Ujumbe #7 **Alla kumbe umo!**

Ujumbe #11 **kwako mtu hanitoi.**

Katika sentensi za hapo juu tunaona kuwa zimesheheni kiima kimoja yaani sehemu ya kwanza inayotoa wazo na kasha kuwa na kiarifu kinachoeleza zaidi kuhusu kiima.

- **Sentensi Ambatani**

Massamba (2009) anaifafanua sentensi ambatani kama inayotokana na kuunganishwa kwa sentensi mbili ambazo kila moja inajitegemea kimaana. Sentensi ambatani aghalabu huweza kuunganishwa na kiunganishi. Katika data yetu ya jumbe madukani tulipata mifano hii:

Ujumbe #19 **Usijifanye machachari kumbe mwandishi wa habari.**

Ujumbe #22 **Nimewapa shua sasa mnaweza kuamua.**

Katika mfano wa kwanza, tunaona sentensi mbili zikijitokeza zilizo unganishwa na kiunganishi kumbe na unapo zitazama utaona kuwa kila sentensi inaweza kujisimamia kimaana. Hali hiyo pia inajitokeza katika sentensi ya pili ambapo kiunganishi sasa kimeweza kutumika kuziweka pamoja sentensi hizo mbili zilizojitegemea kimaana. Ni muhimu kufahamu pia kuwa sentensi ambatani huwa na kiima na kiarifu.

- **Sentensi changamano**

Sentensi changamano ni sentensi ambayo ndani yake kuna kishazi kilicho huru na kishazi kingine ambacho ni kitegemezi.

Baadhi ya mifano tuliyopata katika data yetu ni pamoja na;

Ujumbe #17 **Mambo yangu yamefana, mtabaki kufinyana.**

Ujumbe #21 **Muache upelelezi mengine hamuyawezi.**

Ujumbe #24 **Hata ukinichukia la kweli nitakwambia.**

2.6.2 Msamiati

Kamusi teule ya Kiswahili (2015) inaeleza msamiati kama maneno yote magumu na rahisi ya lugha yoyote inayotumika.

Tumetumia msamiati hapa kwa maana ya maneno magumu yaliyotumika katika jumbe za lesu za kusuta.

Msamati unaotumika katika lesu unategemea na ujumbe husika katika lesu yenyewe. Katika mazingira mengine lazima wasomaji wajikite katika muktadha ili kuweza kuelewa jumbe katika lesu. Katika jumbe za kusuta nilizokusanya kuna misamiati mingi iliyojitokeza ambayo sikuifahamu, ilibidi kurejelea tafiti za awali na pia kuwahoji wenye maduka ya lesu ili kupata maana. Baadhi ya misamiati iliokuwa migumu kuelewa ni pamoja na:-

Mf:2

Ujumbe #10 **habibi- kumaanisha mpenzi.** Maana ya neno hili tuliipata kutoka kwa kamusi teule ya Kiswahili (2015). Habibi ni mtu unayempenda, aliye wa karibu kwa nafsi yako.

Ujumbe # 15 **Unguja na Pemba-Kumaanisha kila sehemu.** Unguja na pemba ni sehemu Fulani zilizoko pwani ya Afrika Mashariki lakini katika muktadha wa ujumbe huu wa lesu Unguja na Pemba zimetumika kwa maana ya kila sehemu na mwandishi ametumia miji hii miwili kama kielelezo cha sehemu tofauti ulimwenguni au labda kurahisisha uelewa wa msomaji ametumia miji iliyo katika sehemu za pwani ya Afrika Mashariki kuliko na wawaaji wengi wa lesu.

Ujumbe # 22 Mwandishi wa habari-Mjuaji au anayetaka

kusema sana. Mwandishi wa habari hapa amechukuliwa kama mtu anayependa kusema sana. Kutokana na muktadha wa ujumbe huu mwandishi wa habari amechukuliwa kama mtu anayetoa maneno kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa nia ya kuchochea ugomvi baina ya watu wawili wanaojuana vizuri.

Ujumbe#24 Nyota ya punda-kumaanisha anayeonewa au asiye na bahati. Kama tujuavyo mnyama punda aghalabu huhusishwa na ubebaji mizigo, katika ujumbe huu nyota ya punda imetumika kuelezea mtu asiye na bahati maishani au anayeishi maisha duni.

Ujumbe #25 Chachandu-maneno au kelele. Hapa chachandu limetumika kuashiria maneno mengi. Mjuzi wa jambo aghalabu huwa mtulivu lakini asiye na ufahamu wa jambo huhusishwa na kusema sana na ujumbe huu unadhihirisha ukweli huo.

Ujumbe #35 Mtachemsha-kumaanisha mtalemewa au yatawashinda. Maana ya neno hili katika muktadha wa ujumbe huu ni kulemewa na si kama tunavyolielewa neno kuchemsha kwa maana ya kuweka motoni na kutokosa.

Ujumbe #36 bata mzoefu wa kupata-asiyeshindwa au mwenye bidii na ukakamavu. Hapa msamiati umetumiwa katika muktadha wa ujumbe huu kuleta maana ya mtu mwenye bidii na wala si bata ndege tunayemjua.

Ujumbe #39 kuosha-kutunza au kulinda. Kuosha ni kusafisha na aghalabu tunaposafisha vitu tunavitunza. Katika muktadha wa ujumbe huu neno hilo kuosha limetumika kwa maana ya kumlinda au kumtunza mpenzi wako kwa kuhakikisha umeyakimu mahitaji yake yote na asiye fanya hivyo huenda akaachwa.

Ujumbe 354 Msabasi-mdaku au mmbeya. Maana ya neno hili tuliipata kutoka kwa Kamusi Teule ya Kiswahili (2005).

Ujumbe#56 golikipa-anayetaka kujua ya watu kila wakati. Golikipa ni mchezaji mpira aliye na jukumu la kuzuia mpira kutoingia wavuni. Katika muktadha wa ujumbe huu ni mtu anayependa kudakia maneno kila wakati na mwandishi amemfananisha na tabia ya golikipa anayedaka mpira wavuni.

Ujumbe #60 **Si chungwa si pera-Si baya si zuri/ si hili wala lile.** Chungwa na pera ni matunda tofauti. Mwandishi wa ujumbe huu hapa anajaribu kuonyesha tofauti ya mambo tofauti kwa kutumia matunda haya mawili.

Ujumbe#61 **Waalimu-wanaojua au wanaofahamu.** Waalimu hapa limetumika kwa maana ya wajuzi au walio na ufahamu wa jambo Fulani kama walivyo walimu na jinsi huwa na ufahamu wa kiusomi.

Ujumbe #63 **chokochoko-maneno mengi.** Mwandishi wa ujumbe huu ametumia neno hili kwa maana ya maneno mengi ambayo mara nyingi huleta madhara.

2.6.3 Matumizi ya Takriri

Mbinu ya kurudiarudia maneno ili kuleta athari katika akili kwa kuisitiza jambo (Kamusi Teule ya Kiswahili 2015)

Inaweza pia kuitwa ukariri. Ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kuisitiza ujumbe fulani. Katika uandishi wa jumbe za kusuta katika lesio tulikumbana na matumizi ya takriri na mifano ni kama ifuatayo;

Mf3

Ujumbe #19 –**nacheka nao nasema nao lakini sina hamu nao.**

Ujumbe#63-**chokochoko si njema.**

Ujumbe #75-**chocha chocha mchochee pweza mwanadamu hamtomweza.**

Ujumbe#83-**Pekepeke za jirani hazinitoi ndani.**

Hapa tunaona maneno yanayorudiwarudiwa ili kuleta msisistizo katika jumbe hii. Maneno yaliyokaririwa ni chokochoko,chochachocha na pekepeke mtawalia.

2.6.4 Matumizi ya maswali ya balagha

Kamusi Teule ya Kiswahili (2015) inaeleza balagha kama neno linalotumika katika misemo kwa maana ya swali lisilohitaji jibu.

Maswali ya balaghani maswali yasiyohityaji majibu. Maswali haya aghalabu hutumiwa kuchochea hisia tofauti miongoni mwa wasomaji au kuteuwa ufahamu wa jumbe husika bila ya kuhitaji jibu hususan. Katika jumbe za kusuta tulizokusanya tulikumbana na jumbe zilizosheheni maswali ya balagha. Kwa mfano;

Mf4

Ujumbe#25 kama we mjuzi chachandu za nini?

Ujumbe #12 Wote waseme hata nawe pia?

Ujumbe #54 Kama si wewe msabasi tungejuajae?

Ujumbe#88 Mgeni si wako Jamvi la nini?

Ujumbe #91 Tangu umeanza umbeya umevuna nini?

2.7 Sababu za kushiriki katika uandishi wa jumbe za kusuta kupitia lesa

Sababu ambazo huwafanya watu kushiriki katika maandishi ya jumbe za kanga haswa zile za kusuta ni nyingi, kama vile walivyo waandishi ama watunzi wenyewe. Kwanza kuna waandishi wanaojichukulia kuwa wao ni wanasanaa. Hawa aghalabu lengo lao huwa ni kutambulika na kujitangaza. Mfano katika maandishi ya jumbe za kanga, wanasanaa hawa hulipwa kwa kupeleka jumbe husika katika maduka ya lesa hivyo basi kuitumia kama njia ya kupata ajira. Waandishi wengine huandika ili kujieleza kimawazo au kihisia. Watu wengine hushiriki katika jumbe hizi kwa njia ya kuwasiliana. Wengine huandika kukashifu uozo katika jamii kama vile wivu chuki na hata mifumo mibaya ya kisiasa.

Kimsingi jumbe katika kanga ni kiwakilisho cha sauti za wanajamii. Wanajamii huandika maoni, mawazo na hata hisia zao kuhusu maishana jinsi wanavyohusiana na wengine katika jamii. Hivyo ndivyo hali ilivyo katika kanga zenye jumbe za kusuta. Wanawake huvaliana kanga hizi ili kupitisha jumbe na masuala tofauti yanayowaathiri katika ulimwengu wao. Kanga zinakuwa ndio njia mwafaka ya kujieleza. Wanawake hawa wana ufahamu kuwa kanga ndilo vazi lililopewa hadhi ya juu na mwanamke hivyo basi kupitia kwake ujumbe husika huweza kupitishwa kutoka mhusika mmoja hadi mwingine. Kanga huvaliwa mara nyingi nyumbani na mazingira yake yamejaa majirani, na hali ya utangamano huwepo, hivyo basi kuwa na uwezekano mkubwa wa kupitisha ujumbe.

Kwa Mfano, Mwanamke aliyevalia lesa iliyoandikwa;

Mf 5

Ujumbe #52-Sikuzoea umbeya jirani sitaki mazoea.

Ujumbe huu unamfahamisha jirani husika kujitenga na kutoleta ushirikiano wa karibu kwani mhusika anajieleza kuwa mtu wa aina gani

Ujumbe# 32-Wapendanao ni sisi hebu tupeni nafasi.

Ujumbe huu unaashiria mapenzi ya hali ya juu na mhusika hapa ana madhumuni ya kutaka kujieleza hadharani jinsi anavyohisi kimapenzi

Ujumbe#98-Sitalipiza lakini sitasahau.

Hapa ujumbe huu Unaashiria mawazo ya mhusika kuhusiana na jamabo fulani. Mawasiliano hapa yamekamiliwa kwani ujumbe aliyodhamiria kuupitisha ni dhahiri.

2.8 Hitimisho

Katika sura hii tunaona kuwa historia na maendeleo ya lesa ni muhimu katika kuelewa vazi hili. Ni dhahiri pia jumbe katika lesa ndiyo sauti ya mwanamke. Mwanamke hutumia jumbe katika lesa kuondoa shinikizo linalotokana na kutopewa nafasi yakujisemea na kujitetea katika jamii. Jumbe hizi hushughulikia masuala ibuka yote katika jamii bila mipaka.

Imedhihirika kuwa lesa ni za aina nyingi na jumbe zake vilevile kwa hivyo hatuwezi kuiwekea mipaka Sanaa hii. Vilevile waandishi wa jumbe za lesa wana ubunifu wa hali ya juu kutokana na uhuru wa matumizi ya lugha waliyonayo.

SURA YA TATU

UAINISHAJI WA MAUDHUI YA JUMBE ZA KUSUTA KATIKA LESO

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeainisha data katika makundi ya kimaudhui na kubainisha ni maudhui gani yanatawala katika jumbe za kusuta katika lesu. Maudhui tawala ni yale ya kusuta, umbeya na mapenzi. Maudhui haya yanafuatiwa nay ale ya kejeli, bidii, unafiki, chuki, ujasiri, wivu wema, tama, usaliti ushirikina na umaskini mtawalia kama tutakavyoona katika jedwali hapo chini.

3.1 Uainishaji wa jumbe kimaudhui katika jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa

Katika utafiti wetu tumechunguza maudhui ambayo yamejitokeza katika jumbe za kusuta za lesu. Jumbe hizi tumeziainisha kimaudhui katika jedwali 1 lifuatalo. Jumbe hizi tumezigawa katika maudhui kama ifuatavyo:-Kusuta, kejeli, ujasiri, umbeya, bidii, unafiki, chuki, mapenzi, wivu, wema, tamaa usaliti, ushirikina na umaskini mtawalia.

Lengo letu katika kujitokeza na maudhui haya limekuwa kubainisha maudhui ambayo yanatawala katika uainishaji wa jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa. Tumefanya hivi kwa kutumia jumla ya asilimia ya matokeo kama inavyoonekana katika jedwali.

Jedwali: Uainishaji wa Maudhui

JUMBE	DUKA	Kusuta	Unafiki	Umbeya	Umaskini	Ujasiri	ivipenzi	Iamaa	Kejen	bigii	enuki	Usani	wivu	wema	Ushirikina
1	Francis	✓													
2	Francis									✓					
3	Francis											✓			
4	Francis		✓												
5	Francis													✓	
6	Francis	✓													
7	Francis	✓													
8	Francis									✓					
9	Francis						✓								
10	Francis						✓								
11	Francis						✓								
12	Francis	✓													
13	Francis						✓								
14	Francis									✓					
15	Francis	✓													
16	Francis		✓												

17	Francis									✓				
18	Francis									✓				
19	Francis		✓											
20	Francis	✓												
21	Francis	✓												
22	Francis			✓										
23	Francis				✓									
24	Francis									✓				
25	Francis	✓												
26	Abdullah	✓												
27	Abdullah										✓			
28	Abdullah					✓								
29	Abdullah							✓						
30	Abdullah								✓					
31	Abdullah	✓												
32	Abdullah							✓						
33	Abdullah				✓									
34	Abdullah	✓												
35	Abdullah				✓									

36	Abdullah								✓					
37	Abdullah						✓							
38	Abdullah	✓												
39	Abdullah						✓							
40	Abdullah									✓				
41	Abdullah			✓										
42	Abdullah	✓												
43	Abdullah									✓				
44	Abdullah													✓
45	Abdullah								✓					
46	Abdullah						✓							
47	Abdullah								✓					
48	Abdullah						✓							
49	Abdullah		✓											
50	Abdullah			✓										
51	Abdullah								✓					
52	Abdullah			✓						✓				

53	Abdullah									✓				
54	Abdullah			✓										
55	Abdullah			✓										
56	Abdullah	✓												
57	Abdullah					✓								
58	Abdullah											✓		
59	Abdullah												✓	
60	Abdullah	✓												
61	Abdullah					✓								
62	Abdullah								✓					
63	Abdullah			✓										
64	Abdullah													✓
65	Abdullah									✓				
66	Abdullah							✓						
67	Abdullah	✓												
68	Abdullah											✓		
69	Abdullah	✓												
	Abdullah													✓

70																	
71	Abdullah	✓															
72	Abdullah						✓										
73	Abdullah					✓											
74	Abdullah	✓															
75	Abdullah					✓											
76	Tanzania							✓									
77	Tanzania								✓								
78	Tanzania	✓															
79	Tanzania		✓														
80	Tanzania								✓								
81	Tanzania									✓							
82	Tanzania	✓															
83	Tanzania				✓												
84	Tanzania		✓														
85	Tanzania										✓						
86	Tanzania														✓		
87	Tanzania							✓									

88	Tanzania	✓														
89	Tanzania			✓												
90	Tanzania			✓												
91	Tanzania			✓												
92	Tanzania									✓						
93	Tanzania								✓							
94	Tanzania	✓														
95	Tanzania			✓												
96	Tanzania	✓														
97	Tanzania								✓							
98	Tanzania														✓	
99	Tanzania										✓					
100	Tanzania			✓												
frik		23	7	15	1	5	13	2	10	8	7	2	3	3	1	
%		23	7	15	1	5	13	2	10	8	7	2	3	3	1	

3.2 Matokeo na Maelezo

Uainishaji wa jumbe kimaudhui umefanywa katika jedwali 1. Tumezianisha jumbe hizi katika makundi 14 kama ifuatavyo:-

Kusuta, umbeya, mapenzi, kejeli, bidii, unafiki, chuki, ujasiri, wivu, wema, tama, usaliti, ushirikina na umaskini.

Kutokana na uchanganuzi wetu wa data matokeo ya makundi haya ya kimaudhui ni kama inavyodhihirisha katika kielelezo 1 kifuatacho:-

Kielelezo 1 : Asilimia za maudhui

Maudhui	Asilimia
Kusuta	23
Umbeya	15
Mapenzi	13
Kejeli	10
Bidii	8
Unafiki	7
Chuki	7
Ujasiri	5
Wivu	3
Wema	3
Tamaa	2
Usaliti	2
Ushirikina	1
Umaskini	1

Kulingana na matokeo haya inadhiirika kuwa waandishi wa jumbe za lesi haswa zile jumbe za kusuta wamejadili sana maswala kuhusu misuto ambayo yameongoza kwa asilimia 23.

Idadi kubwa ya watumizi wa lesi, maeneo ya Pwani ni wanawake na kulingana na mila na desturi za Pwani wanawake hawa hutumia misuto kwa njia ya kupitisha ujumbe kutoka sehemu moja hadi nyingine (Hanby na Bygott 1984). Hivyobasi, kusuta kunajitokeza kama maudhui yanayojisimamia na yanayotawala katika kuainisha jumbe hizo za kusuta. Baadhi ya mambo ambayo yamejadiliwa katika maudhui ya kusuta ni pamoja na:-maadili mema katika jamii kama heshima, ushirikiano kati ya wanajamii na Uvumilivu kati ya wanajamii.

Ukweli huu unaelezwa na mifano ifuatayo;

Ujumbe#6 **Linifikalo niachieni mwenyewe.** Ujumbe uliomo katika maandishi haya ni kutokuwa na tabia ya kutaka kujihusisha na mambo ya watu. Hii ni tahadhari ya wale walio na tabia ya kupenda sana kujihusisha na maisha ya wenzao bila kuzingatia madhara yanayoletwa na tabia kama hiyo.

Ujumbe#15 **Wacheni chenu kiwewe Unguja na Pemba ina wenyewe.** Hapa ujumbe unao jitokeza ni kuwa na makini na ustaarabu unapokuwa mgeni sehemu Fulani kwani kila sehemu ina wenyewe.

Ujumbe#42 **Utamaliza limau dhahabu haiwi almasi.** Ujumbe hapa ni kufahamu kuwa kuna mabo ambayo hayawezi kubadilika kamwe. Hivyo basi kuwaasa wanaopenda kutaka kubadilika mipangilio ya mambo bila kuzingatia sheria zilizowekwa.

Ujumbe#40 **Nimestahimili taabu kupata si ajabu.** Ujumbe huu unaashiria uvumilivu.

Kwa hakika kama inavyoonekana katika data yetu asilimia kubwa ya matokeo ni kuhusu misuto. Hivyobasi, tunaonelea kuwa asilimia hii kubwa ya matokeo kuhusu misuto ni kiashirio kuwa watumizi wa lesi wana mazoea ya kuwasilisha asilimia kubwa ya jumbe kupitia misuto kwa kuchukulia kwamba katika mila na desturi zao kama tulivyotaja awali hutumia misuto kuwasilisha jumbe.

Tukitizama mifano hapo juu tunaona kuwa swala la maadili mema katika jamii linajitokeza waziwazi. Katika Ujumbe#6, Mwandishi mmoja ameandika kuwa “linifikalo niacheni mwenyewe” ambapo mwandishi anaonekana kuwaeleza wanajamii kuwa mambo yanayompata mja huweza kumpata kila mtu, hivyobasi kuwaasa waja kutokuwa na ile tabia ya kujihusisha na maisha ya wenzao. Mfano huu basi unakua kielelezo mwafaka cha maadili mema katika jamii.

Pia waandishi wa jumbe katika lesa wamegusia swala la ushirikiano katika jamii kupitia jumbe hizi za kusuta.

Ujumbe#15 Wacheni chenu kiwewe Unguja na Pemba ina wenyewe

Katika ujumbe huu mwandishi anasisitiza jinsi wanajamii kutoka pande tofautitofauti wana mitazamo tofautitofauti, vilevile jinsi wanavyoishi maisha yao ya kila siku, hivyobasi kuwaasa wanajamii umuhimu wa kushirikiana wakati wanapoingiliana.

Zaidi ya hayo swala la uvumilivu limejitokeza katika jumbe hizi za kusuta. Ujumbe#40 “**Nimestahimili taabu kupata si ajabu**”, unadhihirisha ukweli wa hoja hiyo

Maudhui kuhusu umbeya vilevile yaliyojitokeza ndani ya jumbe hizi za kusuta yanavutia waandishi wengi kwani matokeo yake yanachukua nafasi ya pili kwa asilimia 15

Maswala kuhusu umbeya katika jumbe hizi za kusuta yanaonekana kujitokeza kwa wingi, kwani katika jamii hii ya Pwani aghalabu walitumia mawasiliano ya aina hii (umbeya) kama njia ya kuwasilisha ujumbe. Pengine maandishi katika lesa ndiyo yanayowapa wanajamii mda wa kutosha ili kuweza kuzieleza hisia zao. Watumizi wa lesa kupitia lesa, wanapata ushauri na wengine kutaja mambo ambayo si rahisi kutaja hadharani.

Kuhusiana na umbeya kuna waandishi wanaotumia umbeya ili kuficha aibu, na kuna wengine ambao wanataja masuala kuhusiana na umbeya bila kuficha. Katika data yetu tulipata mifano kama vile:-

Ujumbe #33- usiwajali wambeya kusema wamezoea.

Ujumbe #55- kutwa kucha jina langu midomoni mwenu.

Ujumbe #56- **usijifanye golikipa kila jambo kulidaka.**

Ujumbe #83- **pekepeke za jirani hazinitoi ndani.**

Ujumbe #89- **hasidi jenga shule sabasi asome.**

Kutokana na mifano hii ni wazi kuwa hii ndio taswira halisi ya jamii. Mwandishi wa ujumbe #33- “usiwajali wambeya kusema wamezoea”, anaonekana kuyayapuuza maswala kuhusiana na umbeya kwani anaelewa fika kuwa tabia hii ya umbeya ipo, na hivyo basi kuisusia na kuwapa tahadhari wanajamii kuhusiana na umbeya. Hii ndio picha tunayopata katika jamii.

Vilevile ni wazi kuwa watu wengi katika jamii wanateseka kuhusiana na masuala ya umbeya kwani mara nyingi jumbe hizi huandikwa kwa njia ya tafsida, hivyo basi huona aibu kukabiliana ana kwa ana kwani si dhahiri kama ujumbe huo umekusudiwa nani/nini. Kwa mfano ujumbe #56- “hasidi jenga shule sabasi asome.”

Jumbe hii inadhihirisha ukweli kuwa katika umbeya hakuna nafasi ya makabiliano ya ana kwa ana.

Maudhui yanayochukua nafasi ya tatu ni yale ya mapenzi ambayo yana asilimia 13. Maudhui haya yalivutia maswala ya kimapenzi na mahusiano ya kimapenzi katika makundi tofauti tofauti. Mahusiano ya kimapenzi yana mijadala mingi katika jamii. Tukirejea ujumbe # 32- “wapendanao ni sisi hebu tupeni nafasi”, mwandishi anaeleza kuwa masuala ya mapenzi hayawezi kufichika.

Pia lugha kavu imetumika katika uandishi wa jumbe hizi za mapenzi. Kwa mfano, ujumbe #11- kwako mtu hanitoi.

Ujumbe #29- **nitazidi kumpenda mpate kusema sana.**

Masuala kuhusu mapenzi katika jamii zingine ni miiko yaani hayapaswi kusemwa hadharani. Pengine jumbe hizi katika lesa ndizo zinawapa watumizi wa lesa mda na nafasi ya kutosha ili kueleza hisia zao za kimapenzi.

Kupitia kwa jumbe za lesa watumizi wengine wanatafuta mapenzi na wengine ushauri. Mifano ifuatayo inadhihirisha ukweli huu.

Ujumbe #66 **Mengi yanauma moyo si chuma**

Ujumbe #37 **Sijamtaka nikimtaka namchukua**

Ujumbe #48 **Kama wamridhisha asingenifuata**

Jumbe kuhusu kejeli zimechukua asilimia 10. Kejeli inajitokeza katika jumbe hizi, hivyo basi kuchukuliwa kama maudhui yanayojisimamia. Mifano ya jumbe zinazodhihirisha kejeli ni kama ifuatavyo:-

Ujumbe #80 **Vishindo twavijua kunyamaza tumeamua.** Hapa mhusika anajaribu kuweka wazi nia yake ya kukaa kimya na anatomia ujumbe wa kejeli kudhihirisha nia yake.

Ujumbe#47 **Kama huna mafuta paka mate.** Hapa kejeli inajitokeza kwa jinsi mhusika anaambiwa atumie mate kama mafuta hayapatikani. Kwa ufupi mwandishi anajaribu kutueleza kuwa kunaweza kuwa na njia mbadala za kufanya jambo na lionekane la kupendeza. Kejeli inadhihirika kwa jinsi alivyotumia maneno yake.

Ujumbe#18 **Kohoa uteme tujue ulilonalo.** Mwandishi wa ujumbe huu ametumia kejeli kwa kumshinikiza mhusika aweze kuyasema yalio moyoni mwake, kwa kutumia maneno “kohoa uteme” anadhihirisha kejeli.

Ujumbe#77 **Niteteni mkiniona niambieni.** Ujumbe huu unaleta maana kuwa mhusika anafahamu kuwa watu wanamongea wakati hayupo. Kwa kutaka kuwakejeli anatomia ujumbe kama huu.

Ujumbe#97 **Kero lenu haliwi kikwazo kwetu.** Licha ya bidii ya kutaka kumtatiza mhusika na vijimambo, ujumbe wa kejeli kama huu unatumika kuonyesha kutotatizika na yanayoendelea.

Maudhui kuhusu bidii, unafiki, chuki, ujasiri, wivu, wema, tamaa, usaliti, ushirikina na umaskini hayakuchukua asilimia kubwa sana bali 8%,7%,7%,5%,3%,3%,2%,2%,1%,1% mtawalia. Inonekana watumizi wa lesio hawavutiwi na maswala haya ikilinganishwa na maudhui yanayotawala. Mifano ni kama ifuatavyo;

Bidii

Maudhui ya bidii katika jumbe za kusuta za lesa yalionekana kujitokeza japo si kwa kiasi kikubwa na hivyo basi kuwakilisha asilimia 8 ya jumbe zote kwa ujumla. Mifano iliyojitokeza ni kama ifuatayo:-

Ujumbe #36 **Mimi bata mzoefu wa kupata nikikosa baharini nchi kavu nitapata.** Kutokana na ujumbe huu mhusika anaonyesha bidii ya kutafuta riziki ya kila siku. Anadhihirisha haya kwa kusema kuwa akikosa baharini, nchi kavu atapata kwa maana kuwa akikosa huku atatafuta kule ili mradi aweze kufanikiwa.

Ujumbe#8 **Kila mchukuzi huusifu mzigo wake.** Bidii hapa inadhihirika kwa jinsi ambavyo mwandishi wa ujumbe huu anaeleza umuhimu wa kila kazi kwa kutumia neno mchukuzi na mzigo kama kielelezo cha kazi tofauti na jinsi zinatekelezwa.

Ujumbe#17 **Mambo yangu yamefana mtabaki kufinyana.** Kwa jinsi ambavyo mambo ya mhusika yamefana inaonyesha bidii na ukakamavu kwa yale aliyotaka kukamilisha na hivyo basi kudhihirisha bidii katika ujumbe huu.

Unafiki

Ujumbe#1 **Tenda wema tuwache unafiki.**

Ujumbe#79 **Hapa ni breki kiboko cha wanafiki.**

Ujumbe#84 **Machoni rafiki moyoni mnafiki.**

Mifano hiyo mitatu hapo juu inaeleza matendo ya kinafiki na jinsi ambavyo waandishi wa jumbe hizo wanavyo kikashifu kitendo cha unafiki. Japo kwa asilimia 7, maudhui ya unafiki yaliweza kujitokeza.

Chuki

Maudhui ya chuki pia yalichukua asilimia 7 ya jumbe zote kwa jumla na tulipata mifano ifuatayo:-

Ujumbe#2 **Heri nyuki kuliko chuki.** Hapa mwandishi anajaribu kuonyesha vile kitendo cha chuki ni kibaya na jinsi kinavyoweza kusababisha maafa. Kwa kusema kuwa nyuki ni afadhali mwandishi wa ujumbe huu anadhihirisha jinsi chuki ilivyo mbaya zaidi.

Ujumbe#27 **Hata ukinichukia la kweli nitakuambia.** Ni heri kumueleza mtu ukweli hata akikuchukia ili kukashifu uozo katika jamii. Ujumbe huu unadhihirisha haya.

Ujumbe# 40 **Hasidi hana sababu.** Mtu anayekuchukia anaweza kuwa hasidi wako na pia kukukosesha furaha huwa kazi kwake na ujumbe huu unaonyesha jinsi watu kama hawa hutafuta kila sababu ya kuwakosea wenzao.

Ujumbe#51 **Meli imetia nanga hasidi anatangatanga.** ujumbe huu unatilia mkazo kitendo cha chuki.

Ujasiri

Ujumbe#75 **Chocha chocha mchochee pweza mwanadamu hamtomweza**

Ujumbe#73 **Usinitishie ukame nimezaliwa jangwani**

Ujumbe#57 **Vishindo vya mashua havishtui bahari**

Ujumbe#61 **Nimewashinda waalimu wewe utaweza?**

Mifano ya hapo juu inadhihirisha hali ya ujasiri kwa kueleza jinsi mtu jasiri hatingishiki na vikwazo au changamoto zinazomkabili.

Wivu

Ujumbe#59 **Usinionee wivu bahati kanipa Mungu**

Ujumbe#64 **Acheni firimbi ya wenzenu kuyawekea vitimbi**

Wema

Ujumbe#98 **Sitalipiza lakini sitasahau.**

Tamaa

Ujumbe#76 **Jiko moja halipiki sufuria mbili.**

Ujumbe#30 **Tamaa si asili yangu naridhika na hali yangu.**

Mifano ya jumbe zinazoonyesha maudhui ya tama hapo juu zinakashifu kitendo cha tama na kuonyesha jinsi tamaa si njema.

Usaliti

Ujumbe#49 **Akumulikae mchana usiku atakuchoma.** Ujumbe huu unaonyesha jinsi watu wanavyoweza kubadili tabia zao na kujifanya wazuri wakati mwingine na kubadilika kuwa wabaya wakati mwingine.

Ushirikina

Ujumbe#44 **Si wako pekee yako wengi twamjua**

Kutokana na data hii, ni dhahiri kuwa maudhui kuhusu kusuta, umbeya na mapenzi ndiyo yanayotawala katika jumbe za kusuta katika lesa mjini Mombasa. Matokeo haya yanakubaliana na madhumuni ya utafiti huu kwamba maudhui ya kusuta, umbeya na mapenzi yanatawala katika jumbe za lesa mjini Mombasa. Katika kuhitimisha, ni muhimu kutaja kuwa kuna jumbe ambazo zilikuwa na maudhui ambayo yalichanganyikana kwa kukata kote kote. Hii ina maana kuwa jumbe hizo ziliweza kudhihirisha zaidi ya maudhui moja katika ujumbe husika. Kwa Mfano;

Ujumbe#17 **Mambo yangu yamefana mtabaki kufinyana -Bidii/Wivu**

Ujumbe#37 **Sijamtaka nikimtaka namchukua - Ujasiri/Mapenzi**

Ujumbe#41 **Nikwambie nini na wewe mbeya - Umbeya/Usaliti**

Ujumbe#71 **Mbuzi ashaula mkeka wambeya mtakalia nini? - Umbeya/Kusuta**

Ujumbe#80 **Vishindo twavijua kunyamaza tumeamua – Kejeli/Kusuta/Ujasiri**

3.3 Hitimisho

Katika sura hii tunaona kuwa maudhui kadhaa yamejitokeza japo yale yanayotawala ni yale ya kusuta. Tunaona kuwa japo maudhui ya kusuta ndio maudhui makuu, maudhui mengine madogo yanaonekana kujitokeza katika jumbe hizo za kusuta za lesa kama tulivyozianisha hapo juu. Vile vile jumbe zingine chache zilionekana kusheheni zaidi ya udhui moja na tumeza pia kuzianisha jumbe hizo.

SURA YA NNE

UAINISHAJI WA MITINDO YA LUGHA ILIYOTUMIKA KATIKA JUMBE ZA KUSUTA ZA LESO

4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tumeshughulikia mitindo ya lugha inayojitokeza katika jumbe za kusuta za lesu zilizoko mjini Mombasa. Waandishi wa lesu hutumia ubunifu wao ili kuandika jumbe kwa namna ambayo wataivutia hadhira yao na wakati huo huo kupitisha jumbe.

4.1 Mitindo ya Lugha katika Jumbe za Kusuta za Leso Mjini Mombasa

Uchanganuzi wa matini kimitindo hufanyika katika miktadha ya matumizi ya lugha. (Simpson2004) anaeleza kuwa lugha ni muhimu sana kwa wanaochunguza mitindo kwa sababu maumbo, ruwaza na viwango ambavyo ni sehemu ya muundo wa kiisimu ni muhimu sana katika kudhihirisha uamilifu wa matini husika. Anaonelea kuwa mbinu za kiisimu zenyewe huwa hazileti maana bila kufanyiwa uchanganuzi na kutoa fasiri kuzihusu.

Katika jedwali #2, tunachunguza jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa ili kuonyesha ubunifu wa waandishi wa lesu hizi. Suala la mitindo ya lugha ni pana mno lakini katika utafiti huu tunachunguza mitindo ya kitamathali na ukiushi ambayo ni mitindo iliyojitokeza kwa wingi mno.

JUMBE	DUKA	MAUDHUI	MITINDO		
			TAMATHALI	UKIUSHI	
1	Francis	Unafiki			
2	Francis	Chuki			
3	Francis	Wivu			
4	Francis	Unafiki			
5	Francis	Wema		Semantiki	
6	Francis	Kusuta		Mofolojia	
7	Francis	Kusuta			
8	Francis	Bidii			
9	Francis	Mapenzi			
10	Francis	Mapenzi			
11	Francis	Mapenzi			

12	Francis	Kusuta	Balagha		
13	Francis	Mapenzi		Sintaksia	
14	Francis	Bidii			
15	Francis	Kusuta			
16	Francis	Unafiki			
17	Francis	Bidii			
18	Francis	Kejeli	Chuku		
19	Francis	Unafiki			
20	Francis	Kusuta			
21	Francis	Kusuta			
22	Francis	Umbeya			
23	Francis	Umaskini			
24	Francis	Kejeli			
25	Francis	Kusuta	Balagha	mofolojia	
26	Abdulla	Kusuta			
27	Abdulla	Chuki			
28	Abdulla	Ujasiri	Chuku		
29	Abdulla	Mapenzi			
30	Abdulla	Tamaaa			
31	Abdulla	Kusuta			
32	Abdulla	Mapenzi			
33	Abdulla	Umbeya			
34	Abdulla	Kusuta			
35	Abdulla	Umbeya			
36	Abdulla	Bidii		Semantiki	
37	Abdulla	Mapenzi			
38	Abdulla	Kusuta			
39	Abdulla	Mapenzi		Semantiki	
40	Abdulla	Chuki			
41	Abdulla	Umbeya			
42	Abdulla	Kusuta		Semantiki	
43	Abdulla	Bidii			

44	Abdulla	Ushirikina		Sintaksia	
45	Abdulla	Kejeli			
46	Abdulla	Mapenzi			
47	Abdulla	Kejeli			
48	Abdulla	Mapenzi		Sintaksia	
49	Abdulla	Unafki			
50	Abdulla	Umbeya	Chuku		
51	Abdulla	Kejeli	Takriri		
52	Abdulla	Umbeya			
53	Abdulla	Bidii			
54	Abdulla	Umbeya	Balagha		
55	Abdulla	Umbeya			
56	Abdulla	Kusuta			
57	Abdulla	Ujasiri			
58	Abdulla	Usaliti			
59	Abdulla	Usaliti			
60	Abdulla	Kusuta		Semantiki	
61	Abdulla	Ujasiri	Balagha		
62	Abdulla	Kejeli			
63	Abdulla	Umbeya	Takriri		
64	Abdulla	Wivu		Semantiki	
65	Abdulla	Bidii			
66	Abdulla	Mapenzi			
67	Abdulla	Kusuta	Tasfida		
68	Abdulla	Chuki			
69	Abdulla	Kusuta			
70	Abdulla	Wema		Mofolojia	
71	Abdulla	Kusuta	Balagha		
72	Abdulla	Mapenzi			
73	Abdulla	Ujasiri			
74	Abdulla	Kusuta			
75	Abdulla	Ujasiri	Takriri		

76	Tanzania	Tamaa			
77	Tanzania	Kejeli			
78	Tanzania	Kusuta		Semantiki	
79	Tanzania	Unafiki	Utohozi		
80	Tanzania	Kejeli			
81	Tanzania	Chuki	Utohozi		
82	Tanzania	Kusuta			
83	Tanzania	Umbeya			
84	Tanzania	Unafiki			
85	Tanzania	Chuki			
86	Tanzania	Usaliti			
87	Tanzania	Mapenzi	Tasfida		
88	Tanzania	Kusuta	Balagha		
89	Tanzania	Umbeya			
90	Tanzania	Umbeya			
91	Tanzania	Umbeya	Balagha		
92	Tanzania	Bidii			
93	Tanzania	Kejeli	Chuku.		
94	Tanzania	Kusuta			
95	Tanzania	Umbeya			
96	Tanzania	Kusuta			
97	Tanzania	Kejeli			
98	Tanzania	Wema			
99	Tanzania	Chuki			
100	Tanzania	Umbeya			

Tanbihi

Katika jedwali hili, kuna sehemu ambazo zina mapengo. Mianya hii inawakilisha jumbe ambazo waandishi wake hawakutumia mitindo yoyote ya lugha tunayoshughulikia na ambayo ni ya kitamathali au ukiushi.

4.2 Lugha ya Kitamathali kama Mtindo katika Leso zilizo na Jumbe za Kusuta

Tamathali ni neno au kifungu cha maneno ambacho kina maana iliyofichwa (Wamitila 2003). Tamathali ni mojawapo ya mbinu za matumizi ya lugha ya mkato na ya kisanii. Tamathali hizi humwezesha mtunzi kusema mengi kwa maneno machache yenye mvuto,mguso na mnato. Tamathali za usemi ambazo tumezishughulikia ni pamoja na balagha, takriri, utohozi, chuku na tasfida. Tumezichagua tamathali hizi kwa sababu uchunguzi wetu umeonyesha kuwa tamathali hizi zimetumika kwa wingi katika jumbe za lesotulizokusanya kwa ujumla wake. Tumezijadili tamathali hizi kama ifuatavyo:-

a) Chuku

Kulingana na(Wamitila2003) chuku ni hali ambapo sifa Fulani hukuzwa kupita kiasi. Naye (Mbatiah 2000) anasema kuwa chuku ni matumizi ya lugha ili kutilia chumvi kitu au hali fulani aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Tamathali hii hutumika kuikuza sifa fulani kupita kiasi. Lengo kuu la kutumia chuku ni kulifanya jambo au kitu kionekane kwa udhahiri zaidi. Kwa mfano:-

Ujumbe #18- Kohoa uteme tujue ulilonalo

Mwandishi wa ujumbe “Kohoa uteme tujue ulilonalo” anatilia chuku maneno kwa ujumla wake. Anayalinganisha maneno na kohozi ambalo haliwezi kufichika. Hivyo basi mwandishi huyu anaweza kutoa msisitizo wa ujumbe huo. Chuku hapa imetumiwa na maneno “kohoa uteme” maana ameongeza chumvi kwa kutumia maneno haya ili kutupa picha dhahiri ya ujumbe wenyewe.

Ujumbe # 28- **Naogopa simba na meno yake siogopi mtu kwa maneno yake** ni mfano mwingine wa chuku kwa jinsi ambavyo mwandishi ameyashirikisha maneno ya mwanadamu na meno ya samba.

b) Tasfida

Wamitila (2003) anafafanua tasfida kwa kusema kwamba ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito. Mtumiaji wa tasfida hujiepusha na lugha inayoudhi au ya matusi kwa hivyo tasfida huficha hali fulani ambayo inaweza kuwa na athari fulani isiyokuwa nzuri kwa msomaji au hadhira. Kwa mfano:-

Ujumbe #67- **Hata kwetu wapo....**

Katika ujumbe huu mwandishi ametumia maneno hayo kuficha aina fulani ya watu katika jamii. Aghalabu maneno haya hutumiwa kuashiria watu wenye sifa mbaya katika jamii kama vile wachawi, washirikina , wezi au hata wafisadi.

jumbe # 87- **Heri kumpa jirani kuliko kioze.**

Katika ujumbe huu mwandishi ametumia maneno haya kuashiria kitendo cha ngono. Badala ya kusema waziwazi kwa kutaja mpaka sehemu za siri za binadamu anaziashiria kwa neno kama “kioze”

c) Utohozi

Kulingana na kamusi ya Isimu na lugha (1999) kutohoa ni mbinu ya kuswahilisha maneno ya lugha nyingine yatamkike kama ya Kiswahili. Kwa mfano:

Ujumbe # 79- **Hapa ni breki kiboko cha wanafiki**

Mwandishi wa ujumbe huu ameliswahilisha neno breki kutokana na neno la Kiingereza “brake” lililo na maana ya sehemu ya gari inayotumiwa kusimamishia gari au kupunguzia kasi ya gari.

Ujumbe # 81- **Kama uhasidi ungekuwa na cheo basi ungekuwa dairekta.** Huu ni mfano mwingine wa matumizi ya utohozi katika jumbe za kusuta zipatikanazo kwenye lesa mjini Mombasa.

Neno “dairekta” hapa limetokana na neno “director” la Kiingereza hivyo basi kudhihirisha utohozi. Dairekta ni cheo cha juu katika kampuni au eneo fulani la kazi.

d) Takriri

TUKI (1990) takriri ni mbinu ya kurudia rudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani. Isitoshe takriri inaweza kujitokeza kwa kurudia rudia wazo fulani katika kazi ya sanaa.

Kamusi Teule ya Kiswahili (2015) inaeleza takriri kama mbinu ya kurudiarudia maneno ili kuleta athari katika akili kwa kusisitiza jambo.

Maelezo haya ya mbinu ya takriri yanaonyesha dhana ya urudiaji katika maneno na hata wazo Fulani.

Mfano:-

Ujumbe # 51- **Meli imetia nanga hasidi anatangatanga**

Ujumbe # 63- **Choko choko si njema**

Ujumbe # 75- **Chocha chocha mchochee pweza mwanadamu hamutomueza**

Katika mifano yote mitatu waandishi wametumia takriri ili kuleta msisitizo katika ujumbe unaopitishwa. Maneno yaliyokaririwa ni tangatanga, chokochoko na chochachocha mtawalia.

e) **Balagha**

Kamusi Teule ya Kiswahili (2015) inaeleza balagha kama neno linalotumika katika misemo kwa maana ya swali lisilohitaji jibu.

Maswali ya balagha ni maswali yasiyohitaji majibu. Maswali haya hutumiwa aghalabu kuchochea hisia tofauti miongoni mwa wasomaji au wasikilizaji au kutoa ufahamu wa jumbe husika bila ya kuhitaji majibu hususan.

Jumbe zilizosheheni maswali ya balagha katika jumbe za lesi zilizo za kusuta Mombasa tulizokusanya zilikuwepo kwa mfano:-

Ujumbe # 12- **Wote waseme hata nawe pia?**

Ujumbe # 25- **Kama we mjuzi chachandu za nini?**

Ujumbe # 54- **Kama si wewe msabasi tungejuaje?**

Ujumbe #61- **Nimewashinda walimu wewe utaweza?**

Ujumbe #71- **Mbuzi ashaula mkeka wambea mtakalia nini?**

Kama inavyojidhihirisha katika jumbe hizi,tamathali ya usemi iliyo ya kibalagha aghalabu hujitokeza kama swali lisilohitaji jawabu.

4.3 Ukiushi kama Mtindo

Neno ukiushi katika lugha lilitumika kwa mara ya kwanza na mwanaisimu wa shule ya Prague kwa jina Mukarowsky (1932) kueleza namna lugha ya kifasihi inaweza kutofautiana na matumizi ya kawaida ya lugha,(Thornborrow na Wareign 1998).

Neno ukiushi linatokana na neno “kiuka” linalomaanisha fanya isivyostahili, vunja sheria au fanya makosa (Shake 1999). Shake anaendelea kusema kwamba maingiliano yoyote yanayoathiri lugha kimuundo, kisarafu na hata kimsamiati ambayo yanazivunja sheria za lugha hiyo ni ukiushi wa kimatumizi.

Naye (Mbatiah 2005) anasema kuwa ukiushi ni uvunjaji wa kimakusudi wa kaida za matumizi ya lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza. Hii inamaanisha kuwa msanii anatomia mbinu hii ya ukiushi kuzivunja sheria zilizopo za matumizi ya lugha ili kupata malengo yake katika kazi za kifasihi. Kazungu (1982) ana maoni tofauti na haya ya Mbatiah kwani anauona ukiushi kama mkengeuko, mchepuko au upotovu kutokana na matarajio ya namna ya kufanya mambo.

(Hartman na Stork 1973) nao wanaeleza ukiushi kuwa isilahi inayojumuisha tamko lolote ambalo halifuati kanuni zinazokubalika za kisarafu au miundo ya kisemantiki ya lugha husika. Maelezo ya Kazungu na Hartman na Stork yanalandana kwa kiasi kikubwa kinyume na mawazo ya Mbatiah.

Ukiushi wa kisarafu huwa unatokea katika viwango mbalimbali kama vile; kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki, kimsamiati na kisintaksia. (Thornborrow na wareign 1998) wanasema kuwa tukielewa sheria za kisarafu basi tunaweza kuchanganua kazi za matini kimtindo. Hii ni kwa sababu kila lugha ina sheria zake.

Ukiushi katika utafiti huu tumeuchukulia kuwa uvunjaji wa kanuni za lugha sanifu uwe wa kimakusudi au bila kujua. Katika sehemu hii tumechunguza ukiushi wa kimofolojia, kisemantiki na kisintaksia.

a) Ukiushi wa kimofolojia

Huu ni uvunjaji wa kanuni zinazotawala uendelezaji wa maneno kama vile;

I. Ufupishaji wa maneno

Ufupishaji wa maneno umechangia pakubwa katika ukiushi huu wa kimofolojia kwa mfano:

Ujumbe # 6- Linifikalo niachieni mwenyewe

Neno linifikalo limefupishwa kwa kuondoa silabi “i” ili kuleta uwiano.

Ujumbe # 25- Kama we mjuzi chachandu za nini?

Badala ya kutumia neno wewe mwandishi amelifupisha likawa “we” katika jumbe hii hivyo basi kudhihirisha ufupishaji wa neno.

Ujumbe # 70- Naishi kingwana jirani staki malumbano

Neno staki huendelezwa kama sitaki kwa kawaida lakini hapa limefupishwa kwa kudondoshwa irabu /i/.

b) Ukiushi wa kisemantiki

Matumizi mbalimbali ya mbinu za lugha yanaweza kufanya neno likachukua maana ambayo ni tofauti na maana ya kawaida. Istiari zilizotumika ni kama vile:-

Ujumbe # 5- Maneno yako asali ukisema hatuna swali

Asali ni chakula kitamu kinachotumiwa na binadamu kwa njia tofauti lakini katika muktadha wa ujumbe huu wa lesa umetumiwa kuashiria utamu wa maneno.

Ujumbe # 15- Wacheni chenu kiwewe Unguja na Pemba ina wenyewe

Hapa matumizi ya miji ya Unguja na Pemba haijatumika kuashiria miji yenyewe bali tajriba ya watu wa jamii fulani.

Ujumbe # 36- Mimi bata mzoefu wa kupata , nikikosa baharini nchi kavu nitapata

Bata ni aina ya ndege lakini katika muktadha wa ujumbe huu neno bata limetumika kuashiria mtu mkakamavu.

Ujumbe # 42- Utamaliza limao dhahabu haiwi almasi

Limao ni aina ya tunda litumiwalo mara nyingi katika upishi lakini katika muktadha huu neno hili limetumika kuashiria uhalisia wa kitu au jambo lisilobadilika. Majina dhahabu na almasi pia yametumika kuashiria uhalisia huohuo.

c) Ukiushi wa kisintaksia

Huu ni ukiukaji wa kanuni za mpangilio wa maneno katika sentensi. Kwa mfano:-

Ujumbe #13- Ni leo hadharani mtu na mtu wake

Mwandishi hapa ameanza sentensi kwa kiunganishi “ni” ambao si muundo unaokubalika katika lugha ya Kiswahili. Muundo huu huweza tu kujitokeza katika kazi za fasihi kutokana na kile kijulikanacho kama idhini ya ushairi.

Ujumbe # 47- Kama huna mafuta paka mate

Ujumbe # 48- Kama wamridhisha asingenifuata

Matumizi ya viunganishi kuanzia sentensi yanajitokeza katika mifano hii hivyo basi kudhihirisha ukiushi wa kisintaksia.

4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tunaona kuwa mitindo ya kitamathali kama vile takriri, balagha, chuku na hata tasfida imeweza kujitokeza. Ukiushi katika viwango vya sintaksia, mofolojia na semantiki pia vimedhihirika kama tulivyoainisha hapo juu katika jedwali. Tunaweza kusema kuwa jumbe hizi za kusuta katika lesa zilisheheni mitindo kadhaa kama tulivyoieleza hapo juu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 UTANGULIZI

Sura hii na ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu, imenuiwa kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu. Kazi yetu imepangwa katika sura tano na katika sura hii tumetoa muhtasari wa sura hizo, tumetathmini nadharia tete za utafiti huu ili kubainisha kama zinaunga mkono au zinapinga matokeo ya utafiti wetu. Mwishowe tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na mada hii ya utafiti.

5.1 Muhtasari

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia utangulizi kuhusu tasnifu hii kwa ujumla.

Sura ya pili tumeangazia suala zima la lesu ambapo tumejadili historia na maendeleo yake, tukaonyesha aina mbalimbali za lesu, pia tumejadili matumizi ya lugha katika uandishi wa lesu na sababu ambazo huwafanya watu kushiriki katika uandishi wa jumbe kwenye lesu.

Katika sura ya tatu, tumeziainisha jumbe za lesu kimaudhui katika makundi yafuatayo: kusuta, umbeya, mapenzi, kejeli, bidii, unafiki, chuki, ujasiri, wivu, wema, tamaa, usaliti, ushirikina na umaskini. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa maudhui ya kusuta na umbeya ndiyo yanayotawala katika jumbe za lesu zilizo za kusuta.

Katika sura ya nne tumefanya uchanganuzi wa mitindo ya lugha ambapo tulikuwa tunachunguza tamathali za lugha na ukiushi. imebainika kuwa tamathali za lugha kama balagha, takriri na utohozi zimetumika sana. Mitindo ya ukiushivilevile imetawala sana katika jumbe hizi za lesu tulizotafiti.

5.2 Hitimisho

Tuliorodhesha nadharia tete tatu kwa ajili ya utafiti huu. Nadharia tete ya kwanza ilidai kuwa maudhui ya ndoa na mapenzi, chuki na wivu yanatawala katika jumbe za kusuta katika lesu mjini Mombasa. Matokeo yanaonyesha kuwa kusuta, umbeya kisha mapenzi ndio maudhui tawala hivyo basi nadharia tete hii si ya ukweli kwani tulichukulia kuwa ndoa na mapenzi, chuki na wivu ndio yanachukua nafasi ya kwanza na pili mtawalia.

Uchanganuzi wetu kuhusiana na nadharia tete ya pili unadhihirisha kuwa ni kweli kuwa lugha za kitamathali zimejitokeza katika mbinu ya kusuta katika kuwasilisha jumbe za lesu mjini Mombasa.

Matokeo ya uchanganuzi wa mitindo ya lugha yanakubaliana na nadharia tete ya tatu kwani matumizi ya tamathali za lugha na ukiushi ni mitindo ambayo inatawala sana katika jumbe za kusuta za lesu mjini Mombasa.

5.3 Changamoto za utafiti

Ni muhimu kutaja kuwa katika utafiti huu tumekumbana na changamoto kadhaa. Kwanza, haikuwa rahisi kuzunguka kwenye maduka ya lesu mjini Mombasa kunukuu na kupata jumbe hizi zilizo za kusuta kwani wenye maduka hawakuwa tayari kushirikiana nasi kutupa jumbe wakichukulia kuwa tulikuwa na madhumuni mengine kama kwenda kuziua jumbe zao kwenye maduka mengine ya lesu mjini. Ilibidi kutoa kitambulisho cha chuo kikuu kudhihirisha kuwa mimi nilikuwa ni mwanafunzi.

Tulipokuwa tukipiga picha tulisumbuliwa sana na walinda usalama wa maduka hayo kwani walidhani sisi ni wanahabari. Baadhi yao walitaka kutotoza ada au tuwahonge ndio tuweze kupiga picha lesu zao.

Muda wa kukusanya data ulikuwa changamoto kwani ilinibidi kusafiri mara kwa mara kuelekea mjini Mombasa ili kuweza kukusanya data hivyo basi kufanya gharama ya utafiti kuwa ya juu. Hata hivyo tulijizatiti na kufanikiwa kumaliza utafiti wetu.

5.4 Mapendekezo

Katika utafiti huu, tulibanwa kwa upeo na mipaka yetu kwani kuna mambo mengi ya kutafitiwa katika eneo hili la jumbe za lesu na ambayo tulibidi kuyaacha nje. Kutokana na utafiti huu tumegundua kuwa lesu zina jumbe nzito na kwa hiyo tungependekeza;

Watafiti watumie njia tofauti za utafiti kama mahojiano ili kupata maoni mbalimbali kutoka kwa watumizi wa lesu.

Utafiti ufanywe katika maduka mengine ya lesu nchini Kenya na kulinganisha matokeo ya tafiti hizo na yale ya utafiti wa sasa.

Tafiti zifanywe kuchunguza sababu tofauti za ubunifu katika duka la Mali ya Abdulla kwani tumegundua kutokana na matokea yetu kuwa jumbe za lesa za Mali ya Abdulla zilikuwa na ubunifu mkubwa zikilinganishwa na jumbe kutoka maduka ya Mali ya Francis na Mali ya Tanzania. Watafiti wachunguze jumbe katika vitabu vya kusoma maktabani.

MAREJELEO

- Atogo (2011) Peace Communications In Kanga: *Kiswahili Research and Communication in East Africa*. Rocha Chimera et al , National Museums of Kenya
- Buliba, A., Mwihaki, A. na Njogu, K (2006) *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Cambridge International Dictionary of English (1995). London: Cambridge University Press.
- Chimera, R. na Njogu, K. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Coulthard, M. (1977) *An Introduction to Discourse Analysis*. Hong Kong: Longman Group Ltd.
- Crystal, D. na Davy, D (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Group Ltd.
- Gallois, C., Giles, H. na Ogay, T. (2007) Communication Accomodation Theory: A Look Back and a Look Ahead. In Gudy Kunst, William B. *Theorizing About Intercultural Communication*. Thousand Oak S,C.A Sage. Pp 121-148
- Johnson- Weiner, K. M. (1998) Community Identity and Language Change in North America Anabaptist communities. *Journal of Sociolinguistics*, 2(3):375-94
- Kihore, Y. M, Massamba, D.P.B and Msanjila, Z. P. (2009) *Isimu Jamii Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: TUKI.
- S. Clark (2005) “ The politics of Pattern: *The Interpretation of Political and Iconography on Kanga cloth*”In H. Aero and Z. Kingdon (Ed), *E.A Contours*. London Horniman museums(2005) Pp 85-97.
- Leech, G.N. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd. Massamba, D.P.B (2009) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mathooko, M. (2007) *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njugu Books.

Mburu, P.N. (2011) *Jumbe Katika Vibandiko vya Matatu*. Nairobi: Tasnifu ya uzamili
Ambayo bado haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Okombo, P.L. (2011) *Sitiara, Taashira na Tashbiha katika Uwasilishaji wa Dhamira
katika Utenzi wa Tambuka*. Chuo Kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya Uzamili
ambayo haijachapishwa.

Shake, R. (1991) *Ukiushi katika Lugha ya Kimaongezi Dhidi ya Kanuni za Kiswahili
Sanifu*. Chuo Kikuu cha Nairobi, Tasnifu ya Uzamili ambayo bado
haijachapishwa.

Simpson, P. (2004) *Stylistics: A Resource Book for Students*. London: Routledge.

Thornborrow na Wareing (1998) *Patterns in Language: An Introduction to Language
and Literary Style*. New York: Routledge.

Toolan, M. (1996) *Language in Literature: An Introduction to Stylistics*. London:
Arnold.

Trudgil, P. (2000) *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. 4th
Edition. London: Penguin Books.

TUKI (2006) *Kamusi ya Kiingereza- Kiswahili*. Toleo la Tatu. Dar es Salaam.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Education
Publishers.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi:
Vide-Muwa publishers.

<http://www.awaazmagazine.com> (Tuesday 1st Nov 2011).

<http://www.glcom.com>- Swahili Language and Culture.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A: DATA YA UCHANGANUZI

Data hii ilikusanywa kutoka maduka makuu ya lesa mjini Mombasa. Maandishi haya yamefifadhiwa katika hali yake halisi na hakuna juhudi zozote ambazo zimefanywa kufanya marekebisho ya tahajia au ukifishi.

Mali ya Francis

1. Tenda wema tuache unafiki
2. Heri nyuki kuliko chuki
3. Haya tena wenye kijicho kazi kwenu
4. Asiye kufaa mvuani usimtumainie juani
5. Maneno yako asali ukisema hatuna swali
6. Linifikalo niachieni mwenyewe
7. Alla kumbe umo!
8. Kila mchukuzi husifu mzigo wake
9. Anayekupenda kweli la machungu hakuelezi
10. Sichoki kukufikiri habibi
11. Kwako mtu hanitoi
12. Wote waseme hata nawe pia?
13. Leo hadharani mtu na mtu wake
14. Uliyoyataka yametimia sasa tulia
15. Wacheni chenu kiwewe Unguja na Pemba ina wenyewe
16. Wote ni wamoja mjinga ni mimi
17. Mambo yangu yamefana mtabaki kufinyana
18. Kohoa uteme tujue ulilonalo

19. Nacheka nao nasema nao lakini sina hamu nao
20. Muache upelelezi mengine hamuyawezi
21. Nimewapa shua sasa mnaweza amua
22. Usijifanye machachari kumbe mwandishi wa habari
23. Maskini hafilisiki
24. Una nyota ya punda kazi yako kubeba mizigo
25. Kama we mjuzi chachandu za nini?

Mali ya Abdulla

26. Asemaye hajapata aliyepata hasemi
27. Hata ukinichukia la kweli nitakwambia
28. Naogopa simba na meno yake siogopi mtu kwa maneno yake
29. Nitazidi kumpenda mpate kusema sana
30. Tamaa si asili yangu naridhika na hali yangu
31. Wakerekao hawamalizi vikao
32. Wapendanao ni sisi hebu tupeni nafasi
33. Usiwajali wambea kusema mamezoea
34. Utakodolea macho hutokijua nilichonacho
35. Mnasema sana sasa mtachemsha
36. Mimi bata mzoefu wa kupata nikikosa baharini nchi kavu nitapata
37. Sijamtaka nikimtaka namchukua
38. Hujakoma tu!
39. Hujui kuosha si ajabu kakutosa

40. Hasidi hana sababu
41. Nikwambie nini na wewe mmbea?
42. Utamaliza limao dhahabu haiwi almasi
43. Ukinipa ntapokea kuomba sikuzoea
44. Si wako peke yako wengi twamjua
45. Endelea mie napumzika
46. Nipe nikupe
47. Kama hauna mafuta paka mate
48. Kama wamridhisha asingenifuata
49. Akumulikaye mchana usiku atakuchoma
50. Taji nimevalishwa wambea tulizeni
51. Meli imetia nanga hasidi anatangatanga
52. Sikuzoea umbea jirani sitaki mazoea
53. Mwenye njaa mshibishe kesho muonyeshe jembe
54. Kama si wewe msabasi tungejuaje?
55. Kutwa kucha jina langu mdomoni mwenu
56. Usiwe golikipa kila jambo kulidaka
57. Vishindo vya mashua havishutui bahari
58. Wakerekao nawazidi kekereka
59. Usinionee wivu bahati kanipa Mungu
60. Si chungwa si pera ni lipi lawakera?
61. Nimewashinda walimu wewe utaweza?
62. Teteni mukichoka niambieni

63. Choko choko si njema
64. Acheni firimbi ya wenzenu kuyawekea vitimbi
65. Nimestahamili taabu kupata si ajabu
66. Mengi yanauma moyo si chuma
67. Hata kwetu wapo...
68. Mwenye chuki hayokewi
69. Asiyesikia huleta majanga
70. Naishi kingwana staki malumbano
71. Mbuzi ashaula mkeka wambea mtakalia nini?
72. Usijipe matumaini sisi hatuachani
73. Usinitishie ukame nimezaliwa jangwani
74. Jeuri dawa yake kiburi
75. Chocha chocha mchochee pweza mwanadamu hutomueza

Mali ya Tanzania

76. Jiko moja halipiki sufuria mbili
77. Niteteni mukiniona niambieni
78. Usishangae na yaliyo nipata ni mkuki humchoma kila mtu
79. Hapa ni breki kiboko cha wanafiki
80. Vishindo twavijua kunyamaza tumeamua
81. Kama uhasidi ungekuwa na cheo basi ungekuwa dairekta
82. Bahati ni upeo sasa ipo kwangu
83. Pekepeke za jirani hazinitoi ndani
84. Machoni rafiki moyoni mnafiki
85. Hasidi ni wewe hili pia walitia mdomoni
86. Hasidi sasa utameza wembe
87. Heri kumpa jirani kuliko kioze
88. Mgeni si wako jamvi la nini?
89. Hasidi jenga shule sabasi asome
90. Si yako usiyakalie kitako
91. Tangu umeanza umbea umevuna nini?
92. Shughuli ni watu na watu ni sisi
93. Utamaliza waganga mimi hunipati ngo!
94. Ulisema hayawi mbona leo yamekuwa?
95. Kama mganga gangua wacha kuyachungua
96. Riziki hutoa Mungu choyo mtakufa nacho
97. Kero lenu haliwi kikwazo kwetu

98. Sitalipiza lakini sitasahau

99. Fitina yako nimegundua kwangu hupati kitu

100. Tatua lako langu halikuhusu.

KIAMBATISHO B: BAADHI YA PICHA ZA KANGA





MAMBO YANGU YAMEFANA MTABAKI KUFINYANA



USIJIFANYE MACHACHARI KUMBE MWANDISHI WA HABARI

